SportPesa
TZS. 537,737,060
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Pinda** awashangaa wanaouza nyumba kugombea ubunge

UKURASA 3




UKURASA 11

Nipashe
Jumamosi Oktoba 2, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580721
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Madiwani watwangana makonde kisa 40,000/-

UKURASA 2



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (mwenye miwani) na wenzake wawili, Silvester Nyegu na Daniel Mbura, wakiwa chini ya ulinzi wa askari magereza wakati wakiingia katika viwanja vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha jana, kusikiliza hukumu ya kesi ya jinai ya unyang'anyi wa kutumia silaha inayomkabili. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Hukumu ya Sabaya yawekwa kiporo

**Hakimu** atoa sababu kuahirishwa, hatima Oktoba 15 ...

*Endelea ukurasa 2*

UKURASA WA 2

## MADEREVA WALIOKWAMA MALAWI SASA WAACHIWA

MADEREVA wa malori ya mizigo wa Tanzania waliokuwa wamekwama kutokana na mgomo uliofanyika nchini Malawi, waliachiwa jana jioni kuendelea na safari. Hatua hiyo inatokana na madereva...



UKURASA WA 3

## TEMBO WABOMOA NYUMBA, WAUA MTOTO

MTOTO mmoja amefariki dunia baada ya nyumba alimokuwa amelala kudondoshwa na tembo katika kitongoji cha Buganza, Kijiji cha Mwanzagamba, Kata ya Mwanyahima...



UKURASA WA 3

## WATU 51 KORTINI TUHUMA UHALIFU, MMOJA KIFUNGO CHA NJE KWA

WATU 51 wamefikishwa mahakamani kwa kipindi cha miezi tisa, mwaka huu, wakikabiliwa na kesi za mbalimbali za...

UKURASA WA 4

## HUKUMU YA AVEVA, KABURU OKTOBA 6

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu inatarajia kutoa hukumu dhidi ya aliyekuwa Rais wa Klabu ya Simba, Evans Aveva na Makamu wake, Godfrey Nyange, maarufu Kaburu Oktoba 6, mwaka huu...



## Wazee walia umbali chanjo ya corona

UKURASA 5

MICHEZO YANGA MOTO ULE ULE KWA GEITA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Madiwani watwangana makonde kisa 40,000/-

**Na Mwandishi Wetu,** KAHAMA

MADIWANI wawili wa viti maalumu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, wametwangana makonde wakigombea Sh. 40,000 muda mfupi baada ya kumaliza kikao cha baraza la madiwani.

Meya wa Manispaa hiyo, Yahaya Bundala, alisema tukio la madiwani hao kutwangana makonde lilitokea akiwa kwenye kikao jijini Dodoma. Aliwataja madiwani hao kuwa ni Violet Bulili na Herither Makaga. Kwa mujibu wa Menya Bundala, chanzo cha madiwani hao kupigana kutokana na Bulili aliyekuwa akimdai Makaga Sh. 40,000 ambazo alitaka alipwe baada ya kikao kumalizika.

"Mimi nilipewa taarifa hizo nikiwa kwenye kikao Dodoma lakini kabla sijazifanyia kazi nikapata safari nyingine ya kwenda Dar es Salaam. Nitawaita madiwani hao waliopigana kwenye kamati ya maadili," alisema Bundala.

Makaga alipoulizwa alikiri kuwa alikuwa akidaiwa fedha hizo na Bulili na alimwambia waende benki akamlipe lakini akakataa na badala yake alianza kumshambulia kwa kumpiga makofi.

"Pamoja na kwamba nilimwambia nitampa pesa zake wako waheshimiwa akiwemo Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba na Michael Mzubo Diwani wa Mhongolo ambao walitoa fedha ili kunilipia lakini Vaileth aligoma na kutaka nilipe mwenyewe," alisema.

Hata hivyo, Bulili alipotakiwa kuzungumzia sakata hilo, alionyesha kutofahamu kilichotokea.

Licha ya kusema hajui, Meya alisisitiza kwamba lazima waitwe wote kamati ya maadili akirudi kutoka Dar es Salaam.




Rais Samia Suluhu Hassan akimsikiliza Mtaalamu Mwandamizi wa Elimu ya Jinsia kutoka Shirika la World Education Inc (WEI), Grace Muro (kushoto), alipotembelea banda la shirika hilo, katika maonesho ya mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO's), jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Hukumu ya Sabaya yawekwa kiporo

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, imeahirisha hukumu ya aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (34), na wenzake wawili hadi Oktoba 15, mwaka huu.

Hukumu hiyo ya kesi ya jinai ya unyang'anyi wa kutumia silaha, ilishindikana kutolewa jana kama ilivyopangwa awali kwa kile kilichoelezwa kuwa maandalizi hayajakamilika. Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine ni Sylvester Nyegu (26) na Daniel Mbura.

Akizungumza mahakamani hapo Hakimu Mkazi Amalia Mushi, alisema: "Maandalizi ya hukumu hayajakamilika, hivyo kesi inaahirishwa hadi Oktaba 15, mwaka huu, hukumu itakapotolewa."

Sabaya na wenzake waliwasili katika viwanja vya Mahakama hiyo majira ya saa 3:45 asubuhi wakiwa kwenye gari aina ya Toyota lenye namba za usajili T233 CXX chini ya ulinzi mkali.

Kabla ya washtakiwa hao kufika, majira ya saa 1:30 asubuhi wananchi walifika viwanja vya mahakama kwa kusikiliza hukumu ya kesi hiyo.

Kadhalika, ulinzi uliimarishwa katika eneo la kuzunguka mahakama hiyo kabla ya washtakiwa kufika huku katika lango la kuingilia mahakamani hapo, walinzi waliwazuia watu ambao wamevaa nguo zisizoruhusiwa.

Baada ya washtakiwa hao kuingia ndani katika chumba cha mahakama majira ya saa 4:00 asubuhi, ndugu, jamaa na marafiki wa Sabaya walibubujikwa na machozi kabla ya hakimu kuahirisha kesi hiyo.

Mawakili wa Jamhuri, Filex Kwetukia, Tersila Gervas na Ofmed Mtenga, waliwasili mahakamani hapo majira ya saa 3:45 asubuhi, huku wale wa utetezi wakiwasili saa 3:20 asubuhi, wakiongozwa na Mosses Mahuna. Wengine ni Duncan Oola na Sylvester Kahunduka.

Awali, mashtaka yaliyosomwa mahakamani hapo, ilidaiwa kuwa washtakiwa kwa pamoja Februari 9, mwaka huu, wakiwa mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba Sh. 2,769,000 mali ya Mohamed Saad na baada ya wizi huo walitumia silaha kuwatisha waliokuwa dukani hapo.

Shtaka la pili ni la unyang'anyi wa kutumia silaha ambapo ilidaiwa kuwa washtakiwa hao kwa pamoja, wakiwa mtaa wa Bondeni waliiba Sh. 390,000 mali ya Bakari Msangi na baada ya wizi huo, walimfunga pingu, wakampiga makofi, mateke, ngumi na wakatumia silaha kumtisha ili wabaki na fedha walizochukua kutoka kwake.

Shtaka la tatu ni la wizi wa kutumia silaha na ilidaiwa kuwa Sabaya na wenzake wawili, Februari 9, mwaka huu, katika Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba simu moja aina Tekno Pop 1 na Sh.35,000 mali ya Ramadhani Rashid.

Baada ya kufanya uhalifu huo, walidaiwa kuwa walimpiga makofi, ngumi, mateke na walitumia silaha kumtisha ili wabaki na fedha na mali walizoiba.

# Madereva waliokwama Malawi sasa waachiwa

**Na Romana Mallya**

MADEREVA wa malori ya mizigo wa Tanzania waliokuwa wamekwama kutokana na mgomo uliofanyika nchini Malawi, waliachiwa jana jioni kuendelea na safari.

Hatua hiyo inatokana na madereva wa nchi hiyo waliokuwa wamegoma, kuwatangazia kuwa wamemalizana na serikali yao.

Akizungumza na Nipashe, mfanyakazi wa kampuni ya Acer Logistic Tanzania, Seleman Mgaza, ambaye ni miongoni mwa madereva waliokwama nchini humo, alisema wametangaziwa na madereva wenzao wa Malawi kuwa wapo huru kutembea.

"Kwa wakati huu (saa 10:43 jioni) nipo eneo la Ikwendeni na walinizuia Mzuzu tangu Jumatatu na wametutangazia dakika 40 zilizopita kuwa matatizo yao yamekwisha. walichotwambia ni kwamba wameshamalizana na serikali yao kwa hiyo tuko huru kutembea Malawi yote," alisema.

Mgaza alisema Alhamis iliyopita, alitoka Dar es Salaam kwenda nchini humo na kwa kawaida huwa wanatumia siku sita mpaka saba kwenda na kurudi kama hakuna vikwazo.

"Nilitoka Dar es Salaam Septemba 23 na nilivuka mpakani Septemba 25 na Septemba 27 nilikuwa Lilongwe lakini ndiyo likatokea hili mpaka leo (jana) bado sijafika Dar es Salaam," alisema.

Juzi, video ilisambaa kwenye mitandao ya kijamii ikionyesha baadhi ya magari yenye namba za usajili wa Tanzania yaliyoegeshwa eneo la Kanengo, Lilongwe nchini Malawi, yakiwa yamevunjwa vioo kutokana na tatizo hilo lililokuwa limetokea.

Balozi wa Tanzania nchini Malawi, Benedict Mashiba, alisema juzi kuwa vurugu hizo zilianza Jumatatu na kwamba madereva wako salama na hakuna taarifa za majeruhi yeyote.

**"Kwa wakati huu (saa 10:43 jioni) nipo eneo la Ikwendeni na walinizuia Mzuzu tangu Jumatatu na wametutangazia dakika 40 zilizopita kuwa matatizo yao yamekwisha. walichotwambia ni kwamba wameshamalizana na serikali yao kwa hiyo tuko huru kutembea Malawi yote," alisema.**

HABARI KITAIFA

# Pinda awashangaa wanaouza nyumba kisa ubunge

**Na Thobias Mwanakatwe,** SONGWE

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amewachana wagombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wanaodiriki kuuza nyumba ili kupata fedha za kugombea ubunge na udiwani na kuonya kwamba ili mtu awe mshindi si lazima awe na pesa.

Pinda aliyasema hayo wakati akizungumza na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Songwe kwenye vikao cha majumuisho baada ya kutembelea wilaya zote za mkoa huu kwa ajili ya kujitambulisha baada chama kumteua kuwa mlezi mpya wa chama mkoa.

"Inapofikia mtu anauza nyumba yake kwa ajili ya kutafuta fedha za ubunge na udiwani halafu chama nacho kinaangalia fedha zimemfanya kufanyia fujo, chama hakimteui na hivyo atanuna miaka 40 maana anaangalia nyumba iko wapi. Sasa nani aliyekwambia ushindi ni pesa tu?" alihoji.

Pinda ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (CC-NEC) ya CCM, alisema kumekuwa na tatizo kwa baadhi ya wanachama hata uchaguzi unapokuwa umekwisha wanaendelea kununa wakati wanatambua kuwa haki ya mwanachama ni kugombea tu lakini suala la kuteuliwa si lake.

"Kwenye uteuzi sisi kina Pinda ndio tunasema huyu hapana, huyu achana naye. Tukishakubaliana kuwa huyu ndiyo anatufaa, tunamrudisha anatoka miongoni mwa kundi la wanachama waliojitokeza kugombea. Kwa hiyo tunachotegemea pale ni kuumia kiungwana," alisema.

Pinda aliwaonya baadhi ya wanachama walioanza kujipitisha na kupanga safu ya wagombea kwenye majimbo na kuwataka kuacha tabia hiyo badala yake waachie wabunge watekeleze majukumu yao mpaka kipyenga kitakapopulizwa kwa kuwa ni muda mfupi sasa tangu uchaguzi mkuu ulipofanyika Oktoba, 2020.

"Uchaguzi mkuu umefanyika hivi karibuni. Leo (juzi) hata miezi 10 hatujafika eti watu wameshaanza kusema eee mara afadhali angekuwa Pinda. Ukiona hivyo ni mwongo, achaneni mambo hayo tuwaache wabunge wafanye kazi," alisema.

Kiongozi huyo pia alisema uchaguzi ndani ya chama na serikali, jambo la muhimu ni watu kusameheana kwa yale yaliyotokea wakati wa uchaguzi badala ya kuweka kinyongo kisichokuwa na afya ndani kwa chama.

Aliongeza kuwa nia ya chama ni kuhakikisha kinaendelea kuwa imara kama chama lakini uimara huo utokane na nguvu kubwa ya chama kwenye mashina.

Kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika 2024, alisema ni wa muhimu sana kwa kuwa serikali za mitaa ni kiungo muhimu na ni msaidizi mkubwa sana wa serikali kuu.

Pinda alisema CCM lazima ijipange katika kuhakikisha wanapatikana viongozi wazuri kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa hasa ikizingatia kuwa wenyeviti wa mitaa na vijiji pamoja na madiwani wote wapo kwenye utekelezaji wa ilani ya CCM.



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam, Jumanne Muliro, akionyesha kwa waandishi wa habari jana, vitu mbalimbali vilivyokamatwa na jeshi hilo, vilivyoibwa katika maeneo mbalimbali ya kanda hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tembo wabomoa nyumba, waua mtoto

**Na Happy Severine,** MEATU

MTOTO mmoja amefariki dunia baada ya nyumba alimokuwa amelala kudondoshwa na tembo katika kitongoji cha Buganza, Kijiji cha Mwanzagamba, Kata ya Mwanyahima, Meatu, mkoani Simiyu.

Kwa mujibu wa wa taarifa iliyotolewa jana na Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Simiyu, Richard Abwao, tukio hilo lilitokea juzi na kusababisha mtoto huyo kupoteza maisha baada ya kudondokewa na matofali ya nyumba waliyokuwa wakiishi.

Kamanda Abwao alisema alisema wanyama hao baada ya kutikisa nyumba wakidaiwa walikuwa wanatafuta chakula aina ya michembe (viazi vitamu vilivyokaushwa), walisababisha matofali kumdondokea mtoto huyo aliyekuwa ndani na kufariki dunia.

Abwao alisema baada ya nyumba hiyo kuangushwa, mama wa mtoto huyo, Kulwa Jisanga (26) alijaribu kumwokoa mwanawe kwa kumpeleka Hospitali ya Wilaya ya Meatu kwa ajili ya matibabu lakini baada ya uchunguzi, daktari alibaini alishafariki dunia.

"Awali mama huyo alikuwa amekimbia na watoto wawili ambao aliwaokoa baada ya tembo kuondoka akakumbuka kuwa kuna mtoto mwingine amelala ndipo alipojaribu kumuokoa jitihada zake hazikufanikiwa" alisema Kamanda Abwao.

Mwili wa marehemu ulifanyiwa uchunguzi na daktari Juma Makungu wa Hospitali ya Wilaya ya Meatu na kukabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya mazishi.

Aidha, polisi wametoa wito kwa wananchi wanaoishi jirani na hifadhi za wanyamapori kuendelea kuchukua tahadhari zinazotolewa na wataalamu, ili kudhibiti tembo kuingia vijijini.

# Watu 51 kortini tuhuma uhalifu, mmoja kifungo cha nje kwa ulawiti

**Na Romana Mallya**

WATU 51 wamefikishwa mahakamani kwa kipindi cha miezi tisa, mwaka huu, wakikabiliwa na kesi za mbalimbali za jinai huku baadhi yao wakihukumiwa kifungo cha miaka 30 jela na mmoja kifungo cha nje.

Aidha, kesi ulawiti zilihusisha watuhumiwa watano na kwamba wawili kati yao walifungwa mwaka mmoja na kulipa faini, mawili wanatumikia miaka 30, huku mmoja alihukumiwa kifungo cha nje na kulipa faini.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu ripoti ya matukio mbalimbali wakiwamo watuhumiwa 76 kwa tuhuma tofauti.

Alisema katika kipindi hicho, kesi zilizofikishwa mahakamani na kufikia hatua ya hukumu kwa makosa ya ubakaji zilikuwa nane, zilizohusisha watuhumiwa wanane ambao watatu walifungwa maisha, watatu miaka 30 jela na wawili miaka 20.

"Kesi 19 zilihusu unyang'anyi wa kutumia silaha, watuhumiwa 33 walikutwa na hatia na walihukumiwa miaka 30 jela," alisema.

Muliro alisema kesi za uvunjaji wa nyumba na kuiba zilikuwa tatu zilihusisha watuhumiwa wanne, ambao wawili kati yao walifungwa miezi sita na wenzao miaka mitatu.

Aidha, alisema katika matukio hayo kesi moja ya uvunjaji stoo na kuiba ilifikishwa mahakamani na mtuhumiwa alifungwa miaka mitatu jela.

"Tumepata mafanikio ya kesi moja ya wizi wa mifugo ambapo watuhumiwa 21 walifungwa miaka mitatu jela na kesi nyingine ya kupatikana na silaha ilifikishwa mahakamani na mtuhumiwa alihukumiwa miaka mitano jela," alisema.

Kamanda Muliro alisema watuhumiwa wengine 76 wanaowashikilia miongoni mwao wanadaiwa kujihusisha na wizi wa magari na vifaa vya magari, wizi wa pikipiki, ukwapuaji mikopa, unyang'anyi wa kutumia silaha.

## Hukumu ya Aveva, Kaburu Oktoba 6

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu inatarajia kutoa hukumu dhidi ya aliyekuwa Rais wa Klabu ya Simba, Evans Aveva na Makamu wake, Godfrey Nyange, maarufu Kaburu Oktoba 6, mwaka huu.

Uamuzi huo wa Mahakama umefikiwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba baada ya washtakiwa kufunga ushahidi wao wa utetezi.

Upande wa mashtaka katika kesi hiyo ulikuwa na mashahidi 10 na upande wa utetezi mashahidi wawili ambao ni washtakiwa.

Katika kesi hiyo, washtakiwa walikuwa watatu, ambao Aveva, Kaburu na Zacharia Hans Poppe, ambaye alifariki dunia Septemba 10, mwaka huu.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka saba likiwamo la matumizi mabaya ya madaraka.

Katika shtaka ya kwanza, Aveva na Kaburu wanadaiwa kula njama ya kutenda kosa la matumizi mabaya ya madaraka.

Aveva na Kaburu wanadaiwa kutumia vibaya madaraka yao kwa kuandaa fomu ya kuhamisha fedha Dola za Marekani 300,000 kutoka kwenye akaunti ya Simba iliyoko benki ya CRDB Tawi la Azikiwe kwenda kwenye akaunti binafsi ya Aveva benki ya Barclays.

Pia Aveva na Kaburu wanadaiwa kwa pamoja walighushi nyaraka iliyokuwa ikionyesha Simba inalipa mkopo wa Dola za Marekani 300,000 kwa Aveva kitu ambacho si kweli.

Aveva pia anadaiwa katika benki ya CRDB kutoa nyaraka ya uongo ikionyesha Simba wanalipa mkopo wa Dola za Marekani 300,000.

Pia anadaiwa kuwa katika Benki ya Barclays, Tawi la Mikocheni, alijipatia Dola za Marekani 187,817 wakati akijua zimetokana na kughushi.

Kaburu anadaiwa kumsaidia Aveva kujipatia Dola za Marekani 187,817 kutoka kwenye akaunti ya Simba wakiwa wanajua fedha hizo zimetokana na zao la kughushi.

Aveva, Kaburu na Hans Poppe walikuwa wanadaiwa kughushi hati ya malipo ya kibiashara wakionyesha kwamba nyasi bandia zilizonunuliwa na Simba zina thamani ya Dola za Marekani 40,577 huku wakijua kwamba si kweli.

Aveva anadaiwa kuwasilisha hati ya malipo ya kibiashara ya uongo kwa Levison Kasulwa kwa madhumuni ya kuonyesha kwamba Simba wamenunua nyasi bandia zenye thamani ya Dola za Marekani 40,577 Pia Aveva, Kaburu na Hanspope wanadaiwa kuwasilisha nyaraka za uongo kuonyesha kuwa Simba imenunua nyasi bandia zenye thamani ya Dola za Marekani 40,577.

## Anusurika kuchomwa moto kisa wizi mzani wa kupimia korosho

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa kijiji cha Mkolopola, Masasi mkoani Mtwara, Hamisi Ajili, amenusurika kufa kwa kuchomwa moto kutokana na kupigwa na wananchi wenye hasira baada ya kukutwa akiiba mzani wa kupimia korosho.

Sambamba na mizani hiyo, Ajili alikutwa na zaidi ya magunia 50 ya Chama cha Msingi cha Ushirika (AMCOS) cha Namwanga kilichoko kijiji cha Mkolopola.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mkolopola, Thadeus Nyang'ama, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea juzi majira ya 6:00 usiku

Alisema majira ya saa 6:30 usiku akiwa nyumbani kwake amepumzika, alipokea simu kutoka kwa mwananchi kwamba kuna tukio la wizi wa mizani katika moja ya vituo vya kukusanyia korosho.

Mwenyekiti huyo alisema mtu mmoja ambaye alifahamika kwa majina ya Hamisi Ajili akiwa na wenzake wawili, walifika katika ofisi ya ununuzi na ukusanyaji wa korosho za chama cha msingi cha Namwanga kisha kuvunja kufuli na kuingia ndani. Alisema wananchi walifanikiwa kumkamata mtu huyo huku wenzake wakikimbia.

Alisema baada ya watu hao kuingia ndani, walibeba mzani moja ambao hutumika kupimia korosho za wakulima na kwamba ndani humo pia kulikuwa na magunia 50 ambayo yaliwekwa kwa ajili ya kuhifadhia korosho za wakulima ambazo zitaanza kununuliwa hivi karibuni.

Nyang'ama alisema wakati watu hao wakiwa katika harakati za kubeba mzani huo na magunia hayo, baadhi ya wananchi waliwagundua na kuwavamia na kumshika mmoja na kuanza kumpiga kwa kutumia vitu mbalimbali vikiwemo mawe na magongo.

"Mtu huyu kwa kweli ameumizwa vibaya na amepelkwa katika kituo cha polisi cha wilaya ya Masasi kwa ajili ya usalama wake," alisema Nyang'ama.

Mwenyekiti wa Chama cha Msingi Namwanga, Noel Millanzi, alisema ni kweli kumetokea tukio la mkazi huyo kukamatwa akiwa anaiba mzani wa chama cha kupigwa na wananchi.

Alisema kabla ya kutokea kwa tukio hilo, hivi karibuni kulisambaa vipeperushi vinavyoashiria kuwapo kwa taarifa zinazolenga kutaka kuwachafua viongozi wa chama hicho.

Naye katibu wa Amcos hiyo, Fadhili Lipende, alisema baada ya mtu huyo kukamatwa na kupigwa vibaya hadi kuumizwa mkono na maeneo ya kichwani, wananchi hao walitaka kumchoma moto lakini ilishindakana.

Mapema mwaka huu, katika kata hiyo ya Namwanga Kijiji cha Mkolopola, kulitokea tukio la kukatwa kwa zaidi ya mikorosho 50 ya diwani mstaafu wa kata hiyo, Edwin Kasembe na wananchi wamendelea kujiuliza kuhusu mfululizo matukio hayo.

Jeshi la Polisi mkoani Mtwara limethibitisha kutokea kwa tukio hilo la mtu mmoja kutaka kuiba mzani na kueleza kuwa uchunguzi unaendelea .







## Watumishi halmashauri ya Bunda wasimamishwa kazi

**Na Ahmed Makongo**, BUNDA

BARAZA la Madiwani katika Hamashauri ya wilaya ya Bunda, limewasimisha kazi watumishi 11 kwa tuhuma mbalimbali, ikiwamo ya kushindwa kusimamia ipasavyo makusanyo pamoja na matumizi mabaya ya fedha za miradi ya maendeleo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, Charles Manumbu, alisema juzi kuwa watumishi hao wamesimamishwa kazi kupitia azimio lililotolewa kwenye kikao cha baraza la madiwani kilichofanyika katika mji mdogo wa Kibara, wilayani hapa.

Makamu Mwenyekiti wa Halmahauri hiyo, Keremba Irobi, alisema kuna ubadhilifu mkubwa uliofanywa na baadhi ya watumishi hao kwenye baadhi ya miradi na kwamba wamesimamishwa kazi kupisha uchunguzi utakaofanywa na tume itakayoundwa.

Irobi alisema hali hiyo ilibainika baada ya kamati ya fedha kutembelea miradi na kutokulidhika na utekelezaji wake ndipo ikaundwa kamati ndogo. Kamati hiyo ilipeleka taarifa yake kwenye baraza la madiwani na kutoa uamuzi wa kuwasimamisha kazi watumishi hao.

Alitoa mfano wa fedha zinazodaiwa kutumika vibaya Sh. milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa shule katika kata ya Kitare, Sh. milioni 500 zilizoletwa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya pamoja na Sh. bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala.

Irobi aliwataja watumishi waliosimamishwa kazi kuwa nipamoja na Stephen Ochien'g, Clevanc Bulemo na Sunday Godfrey kutoka idara ya mifugo na uvuvi) kwa tuhuma za kutokusimamia mapato ya samaki, kupokea pesa kama faini na kutoziwasilisha kunakohusika kisha kuzitumia kama mali yao.

Kwa idara ya elimu, waliosimamishwa ni Ofisa Elimu Msingi, Leonald Richard, Kaleja Buyagu na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kitare, Bilomo Mwigembe ambao wote kwa pamoja wanadaiwa kusimamia ujenzi wa shule mpya ya Kitare iliyotengewa Sh. milioni 400.

Katika kitengo cha ununuzi, aliyesimamishwa ni Emmanuel Mboje na katika idara ya ujenzi ni Laurent Marashi na Annastazia Mathias, ambao wote kwa pamoja wanatuhumiwa kutosimamia vizuri ujenzi wa wodi tatu za wagonjwa katika mradi wa hospitali ya halmashauri, uliotengewa Sh. milioni 500, pamoja na jengo la utawala lenye Sh. bilioni moja.

# Wazee walia umbali chanjo ya corona

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZEE mkoani Shinyanga, wamelalamikia umbali wa vituo vya afya ambavyo wamedai vimesababisha kushindwa kupata kwa wingi chanjo ya corona.

Katibu wa Baraza la Wazee mkoani Shinyanga, Anderson Lyimo, alibainisha hayo jana wakati akisoma taarifa ya wazee mkoani hapa kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani yaliyofanyika kimkoa wilayani Kahama katika kijiji cha Nyandekwa.

Alisema wanampongeza Rais Samia Suluhu Hassani kukubali Watanzania kupatiwa chanjo ya corona ili kuwalinda na janga hilo pamoja na kutoa kipaumbele kwa wazee kupatiwa chanjo hiyo.

"Wazee wengi bado hawajapata chanjo ya corona na hii inatokana na umbali mrefu wa vituo vya afya. Tunaomba serikali itusogezee huduma hii ya chanjo iwe karibu ili wananchi na wazee wapate chanjo kwa wingi," alisema Lyimo.

Aidha, alisema licha ya serikali kuendelea kutatua changamoto mbalimbali za wazee, bado wanakabiliwa na ukosefu wa dawa za magonjwa ya wazee kwenye huduma za kiafya.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati, aliwataka wananchi mkoani hapa kupuuza maneno ya upotoshaji kupata kuhusu chanjo ya corona bali wajitokeze kwa wingi kupata chanjo hiyo ili kuwa salama pale watakapopata maambukizi ya ugonjwa huo.

Nao baadhi ya Wazee ambao walijitokeza kupata chanjo ya corona kwenye maadhimisho hayo, walisema wameamua kuchanjwa kutokana na awali hawakupata sababu ya umbali mrefu wa vituo vya afya.

Naye Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Yudas Ndungile, alisema watu ambao yatari wameshapata chanjo ya corona mkoani hapa ni 10,000 na kwamba mkoa ulipatiwa dozi 25,000 kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.



Ofisa Habari wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Zuhura Mtatifikolo, akitoa elimu kuhusu masuala ya Bunge kwa wanafunzi wa shule ya msingi ya Kihonda Maghorofani ya Manispaa ya Morogoro, wakati maofisa wa Bunge kitengo cha elimu kwa umma walipotembelea shuleni hapo juzi. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Wavamizi eneo Chamwino watakiwa kuondoka

**Na Munir Shemweta, WANMM**

DODOMA

SERIKALI imeagiza wananchi waliovamia eneo la Farm katika kijiji cha Chamwino Ikulu mkoani Dodoma kuondoka ndani ya wiki mbili kuanzia Oktoba 2, mwaka huu.

Imeelezwa kuwa kijiji hicho kilishatangazwa eneo la mpango mwaka 1992 kupitia GN Na 263 ya Juni 25, 1992 ili kuepusha Sheria ya Ardhi ya Vijiji (Sura 114 Toleo la 2002) kutumika.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya, wakati wa kutangaza uamuzi wa timu ya uchunguzi wa mgogoro wa eneo la Farm mbele ya wananchi wa kijiji cha Chamwino.

"Natoa tamko la serikali kwa niaba ya kamati ya ulinzi ya wilaya na wananchi wa kijiji cha Chamwino, naagiza wanaokalia maeneo ndani ya eneo la Farm kuondoka ndani ya wiki mbili na watakaokaidi hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao" alisema Msuya.

Sehemu ya eneo la shamba la Farm lenye ukubwa wa ekari 640 lililoanzishwa kati ya mwaka 1971/72 na Hayati Baba wa Taifa, Julius Nyerere, kwa lengo la kuwafunza wanakijiji cha Chamwino ufugaji wa kisasa wa ng'ombe wa maziwa, mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku, lilivamiwa na kuzua mgogoro kati ya wananchi na serikali.

Kwa mujibu wa Msuya, mwananchi yeyote aliyeingia ndani ya eneo hilo ni marufuku kufanya shughuli yoyote kama vile ujenzi, kilimo na serikali kupitia idara ya ardhi itaweka mabango kuonyesha kuwa eneo hilo ni la umma.

"Wanaoendelea kufanya ujenzi watakuwa wanajiingiza kwenye hasara na mwananchi yeyote mwenye nyaraka za kumilikishwa sehemu ya eneo hili afike ofisi ya mkuu wa wilaya na atapatiwa haki yake," alisema.

Kamishna wa Ardhi, Nathaniel Nhonge, alisema kumbukumbu katika eneo hilo zimeweka bayana kuwa eneo lenye mgogoro la Farm lilitolewa kwa matumizi ya umma na hakuna mabadiliko yaliyofanyika kwenda kwa mtu mmoja mmoja.

"Kimsingi hakuna mtu aliyelipwa fidia ndani ya eneo la Farm na wale wananchi waliolipwa kimakosa wanatakiwa warejeshe fedha," alisema Nhonge

Alisema baada ya ripoti ya tume ya uchunguzi kuhusiana na mgogoro huo, sasa upimaji utafanyika eneo lililotolewa kwa matumizi ya taasisi za shule ya sekondari Chamwino, Shule ya Msingi Kikwete na eneo la Mahakama na kuyamilikisha kwa wahusika kuepuka migogoro hapo baadaye.

"Serikali itaweka utaratibu wa kudumu wa kubaini na kulinda maeneo mengine ya aina hii yaliyoko ndani ya Chamwino dhidi ya uvamizi wa wananchi," alisema.

Hata hivyo, baadhi ya wananchi wa kijiji cha Chamwino wameonyesha kutoridhishwa na uamuzi huo kwa madai kuwa maeneo hayo walirithi na kuridhiwa na serikali ya kijiji kwa nyakati tofauti ingawa hawakuwa na nyaraka zozote zinazoonyesha kumilikishwa.

Eneo la Farm katika kijiji cha Chamwino limekuwa kwenye mgogoro wa muda mrefu uliosababisha kuundwa kwa timu maalum ya kushughulikia mgogoro huo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu, wachezaji Bara wanatakiwa kutobweteka

**LIGI** Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa 2021/22 ambayo hutoa wawakilishi wa nchi katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika imeingia katika raundi la pili.

Katika raundi ya kwanza kuna timu ambazo zilipata ushindi, nyingine zilitoka sare na zilizobakia zilipoteza pointi tatu muhimu kwenye michezo hiyo ya ufunguzi.

Majigambo na huzuni vimeonekana kutawala katika baadhi ya timu kutokana na matokeo ambayo wamepata kwenye mechi zao za ufunguzi ambazo zilimalizika Jumatano iliyopita.

Ni jambo la kawaida kwa timu iliyopata ushindi kuanza majigambo kwa kuamini iko katika nafasi nzuri zaidi ya kutwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu kwa sababu iliondoka na pointi zote tatu muhimu.

Timu iliyoshinda inaamini kwamba ilifanya maandalizi sahihi kuanzia kwenye mchakato wa usajili hadi katika kucheza mechi za kirafiki na matokeo waliyopata wamestahili na hivyo wana haki ya kushangilia na kuwabeza wale waliopoteza mechi au walioanza msimu kwa kugawana pointi.

Na kwa upande wa waliotoka sare, iwe ya mabao au ya bila kufungana, wanadhani kuna mahali ambapo walikosea na hicho ndio kimesababisha kukosa ushindi kwenye mchezo huo wa awali.

Lakini kwa timu zilizopoteza mechi zinaonekana kama hazikujiandaa vyema, hazikufanya usajili mzuri na wa kuzingatia mahitaji halisi huku zikionekana huenda pia zinafundishwa na makocha ambao hawana uwezo wa kushindana.

Nipashe tunawakumbusha viongozi na timu zote 16 zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kukumbuka ndio kwanza kipenga kimelia, matokeo ya mechi za raundi ya kwanza yasiwafanye wakabweteka na kujisahau na maandalizi ya mechi zinazofuata.

Timu zinatakiwa kuendelea kujiandaa na kujiimarisha kwa ajili ya mechi zinazofuata na kuzingatia msimu huu ushindani umeongezeka kutokana na zawadi ya fedha zitakazotolewa na wadhamini waliopewa haki ya kuonyesha ligi hiyo kwenye televisheni, Kampuni ya Azam Media.

Tofauti na misimu iliyopita, Azam Media itatoa zawadi ya fedha mpaka kwa timu itakayonusurika kushuka daraja, hii ikiwa ni historia kwenye soka hapa Tanzania.

Lakini wachezaji nao wanatakiwa kujituma kwa ajili ya kutangaza vipaji vyao na kuwavutia makocha wa timu za taifa pamoja na mawakala kutoka sehemu mbalimbali duniani.

Wakati wachezaji na viongozi wakifahamu vyema majukumu yao, waamuzi pia wanatakiwa kuhakikisha wanachezesha kwa haki mechi zote za ligi bila kujali timu au uwanja ambao anafanya kazi.


Mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu zinatarajiwa kuonyeshwa mubashara, hivyo wachezaji wanatakiwa kujituma na si kuchagua baadhi ya mechi, kubagua michezo hakumsaidii mchezaji au timu husika kwa sababu mechi zote zina umuhimu unaofanana.

Ni mapema mno kwa timu kukata tamaa kwa kuangalia matokeo ya mechi ya kwanza, ingawa pia timu hazitakiwi kubweteka kwa kusubiri michezo ya lala salama.

Ushauri huu pia unazihusu timu zote zinazotarajia kushiriki Ligi ya Championship (zamani Ligi Daraja la Kwanza), inayotarajia kuanza kesho, First League (Ligi Daraja la Pili), Ligi ya Mabingwa ya Mikoa na Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Waswahili wanasema biashara asubuhi, jioni mahesabu. Usemi huu unazikumbusha timu na wachezaji wote kuamka mapema kwa kusaka pointi na hatimaye dakika za lala salama kuhakikisha wanakamilisha malengo na si kuwa kwenye nafasi za kujinusuru kuteremka daraja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Ajidhaniaye amesimama aangalie ...

**SHABASHI!** Ajidhaniaye amesimama aangalie asianguke. Maana yake anayejidhania amesimama anapaswa kujiangalia asianguke. Methali hii hutufunza tusiwe na kiburi. Inawakanya wenye vyeo wajichunge kwa kuwa wanaweza kuharibikiwa na kuwa si chochote.

Sasa Yanga wanasema: "Shabashi" (tamko la kupongeza linalodhihirisha hisia ya furaha) baada ya kuifunga Simba na kutwaa Ngao ya Jamii kwa bao moja tu lisilokuwa na jibu lililofungwa na mkongomani Fiston Mayele dakika ya 11 ya mchezo huo.

Ndo maana mimi hukataa kuwa Simba na Yanga eti ni watani wa jadi. Abadan! (tamko la kukataa au kukanusha uwezekano wa kutokea jambo; asilani! Kamwe!) Watani hawadhuriani bali hutaniana na kusaidiana.

Tukubaliane kuwa Simba na Yanga sio watani wa jadi kama isemwavyo bali ni watu wanaowekeana gere yaani choyo kinachoambatana na husuda yaani tabia ya kutopenda mtu mwingine afanikiwe au apate kitu; kijicho, husuda, wivu.

Si Simba wala Yanga inafurahi mojawapo inapokuwa na maendeleo au ushindi. Hata wahenga walisema: "Chuki humchoma anayeihifadhi." Kwa kawaida chuki humsumbua anayeiweka au kuihifadhi. Twafunzwa umuhimu wa kutoiweka chuki kwa kuwa itatudhuru wenyewe.

Hali ilivyo kwa timu hizo mbili nchini ni kwamba kila moja ina jambo la kujiuliza. Kwa nini siku za kumbukumbu zao na kuwaweka hadharani wachezaji waliosajiliwa, uwanja hujaa pomoni yaani katika hali ya kujaa au kuwa -ingi lakini siku timu hizo kongwe zilipopambana kwenye mchezo wa kugombea Ngao ya Jamii uwanja ulipwaya? (kitendo cha kupungua ari ya kutofanya jambo kutokana na kuvunjika moyo) pande zote mbili hazikuwa na uhakika wa ushindi!

Baada ya mechi kumalizika na Yanga kukabidhiwa Ngao ya Jamii baada ya Simba kushindwa kutetea taji hilo kwa mara ya tano mfululizo, ilikuwa ahueni kwa wapenzi wao waliokwepa kuingia uwanjani na sikitiko kwa wenzao wa Yanga waliokacha (kitendo cha mtu kushikilia msimamo au maamuzi yake) kwenda uwanjani kuona jinsi wachezaji wao walivyoshinda na kukabidhiwa Ngao ya Jamii.

Soka, kandanda au kabumbu ni mpira wa miguu. Ni mchezo unaopendwa na kuvuta idadi ya watu wengi zaidi kuliko michezo mingine duniani. Pia ni mchezo unaowatajirisha wachezaji kutokana na mishahara mikubwa wanayolipwa na vilabu vyao.

Kwahiyo haishangazi kusikia mchezaji ana ndege yake binafsi, boti (chombo kidogo cha moto cha kusafiria baharini), majumba ya gharama kubwa, magari kadhaa ya aina mbalimbali, biashara n.k.

Hata kama huku kwetu wachezaji hawalipwi kama wenzao wanaochezea katika mabara ya Ulaya, Brazil, Marekani n.k. lakini pesa wanazolipwa wanapaswa kushukuru Alhamdulilahi, kwani ni neno linalotumiwa kumaanisha kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu; Pia ni tamko la kuonesha shukurani kwa Mwenyezi Mungu kwa jema au baya lililomsibu mtu.

Mashabiki wa Simba na Yanga wapaswa kutambua kuwa adabu ni utaratibu unaokubalika katika kufanya jambo; heshima, nidhamu, tabia nzuri.

Aidha (zaidi ya hayo, vilevile, isitoshe ni neno linalo- unganisha mawazo katika maandishi au mazungumzo.) Kwa hiyo ni muhali yaani jambo lenye ugumu au kutowezekana kwa kuwa mashabiki wa Simba na Yanga kuwekeana au kufanyiana upasi yaani hali ya kutopendana ilhali wote ni Watanzania wanaoishi katika jiji na mtaa mmoja.

Mchezo ni jambo linalofanywa kwa nia ya kuburudisha. Jambo ambalo watu au timu hulifanya kwa kushindana ili kumpata mshindi. Kama ndivyo, kwa nini mashabiki wa Simba na Yanga wachukiane?

Chuki ya kwa nini timu fulani ina maendeleo ni ujinga kwani maendeleo ni hali ya kupata ustawi; ongezeko la ubora katika huduma za kijamii; tendo la kutoka kwenye kiwango cha ufanisi na kufika kwenye kiwango kikubwa.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784334096**

## HABARI KITAIFA

# Wanafunzi kunufaika mgawo taulo za kike

**Na Christina Mwakangale**

KATA ya Saranga katika Manispaa ya Ubungo mkoani Dar es Salaam, itaanza kugawa taulo za kike bure kwa Shule ya Sekondari Saranga, kuanzia mwezi huu, ikilenga kuwaondolea vikwazo wasichana shuleni.

Diwani wa Viti Maalumu, Liberatha Samson, amesema wataanza kwa kuchangishana fedha viongozi wa kata hiyo, huku wakiandaa andiko kwa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kutenga bajeti.

Samson alisema hayo juzi kwenye mafunzo kuhusu bajeti yenye mrengo wa kijinsia kwa madiwani, watendaji kata, wenyeviti wa serikali za mitaa kutoka Kata za Saranga na Mabwepande.

Alisema mafunzo hayo yametoa mwanga na tafakuri kwa viongozi wa mtaa ili kuanza kutatua matatizo ya wananchi wao wenyewe kwa kuweka mikakati badala ya kusubiri bajeti ya serikali.

"Mimi nipo kwenye kamati za huduma za jamii tunaona changamoto nyingi shuleni, hasa zikiwakumba wasichana shuleni kutokana na idadi ndogo ya vyoo, maji na kukosa taulo za kike. Sasa kuanzia Oktoba, tutatoa taulo za kike na baadaye kujadili kutengwa bajeti maalumu kutoka halmashauri," alisema.

Awali, Shakila Mayumana akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ambao wanaratibu mafunzo kwa kushirikiana na COADY International, alisema utendaji wa mzuri wa kiongozi ni ule unaoacha alama katika jamii.

Alisema viongozi wanaoleta mabadiliko kwenye jamii hukumbukwa kwa sababu utatuzi wa matatizo ya wananchi husaidia kuwainua kiuchumi ikiwamo kupunguza umaskini.

"Mafunzo haya yanajenga uelewa wa pamoja kwa viongozi, jamii juu ya umuhimu wa bajeti yenye mrengo wa kijinsia na kupitia bajeti za kata, halmashauri kwa kuzingatia jinsia, vipaumbele," alisema.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo, Deogratius Temba, alisema bajeti yenye mrengo wa kijinsia huondoa migogoro, kuleta usawa, kuondoa mfumo dume na ukatili wa kijinsia.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Tunduru, Augustino Maneno (katikati), akikata utepe kuzindua duka la Vodacom, wilayani humo, mkoani Lindi jana. Kulia ni Mkuu wa Mauzo wa Vodacom Kanda ya Dar es Salaam na Pwani, Brigita Stephen na Mshirika wa kibiashara, Emmanuel Makaki.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watishia kuzuia mradi kisa malipo kiduchu

**Na Juliwaeth Mkireri,** VIGWAZA

WAKAZI wa vijiji vya Mnindi na Visezi katika Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze, wametishia kuzuia ujenzi wa barabara iendayo kwenye mradi wa bandari kavu Kwala endapo hawatarekebishiwa malipo ya fidia kama walivyokuwa wamekubaliana awali.

Wananchi hao walisema hayo jana walipokuwa wakizungumza na waandishi wa habari katika kijiji cha Mnindi kuhusiana na malipo ya fidia kupisha upanuzi wa barabara iendayo katika bandari hiyo.

Walisema wamegoma kutia saini ili walipwe kutokana kukiukwa kwa makubaliano yaliyofikiwa.

Floriana Miho, mmoja wa wakazi wa kijiji cha Mnindi alisema katika makubaliano ya awali ya malipo ya fidia, serikali ilisema itawalipa Sh. 3,800 kwa mita moja ya mraba.

Hata hivyo, alisema walipoitwa kwa ajili ya kutia saini waingiziwe benki fedha zao, walielezwa kuwa wanalipwa Sh. 1,200 kwa mita moja ya mraba jambo ambalo walipingana nalo.

"Kabla mradi haujajengwa tuliitwa kwa maandishi tukajadili kwa pamoja kila hatua na mradi ulipokaribia kuanza, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chalinze alituomba wakati mradi unaendelea tupishe wakati utaratibu wa malipo ukiwa unaendelea. Tulifanya hivyo lakini tumeshangaa leo (jana) tunaitwa kutia saini tofauti makubaliano ya awali," alisema.

Naye Justine Kandoro alisema kitu kinachowafanya wagome kutia saini ili kuingiziwa malipo ya fidia zao ni kushushwa kwa thamani ya ardhi bila maelezo.

Kitungwe Dillala, mkazi wa Visezi alisema mbali na tofauti kwenye malipo pia wako wananchi ambao majina yao yameondolewa kwenye malipo.

Nyaucho John alisema katika kijiji chao cha Visezi watu 11 kati ya 65 ndio watakaolipwa na hadi sasa hawajapewa maelezo kwa nini wengine wameondolewa kwenye malipo ya fidia na endapo hakutafanyika mabadiliko watazuia barabara kuendelea kujengwa hadi watakapolipwa fidia.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mnindi, Juma Omari, alikiri baadhi ya wananchi wake kugoma kupokea malipo waliyoandaliwa kwa madai kuwa yamekwenda kinyume cha makubaliano ya awali.

"Ninachotambua kuna baadhi ya wananchi wangu wamegoma kusaini (kutia saini) wengine wamesaini nilipowauliza wamesema awali walikubaliana

Omari alisema kwa mujibu wa Halmashauri ya Chalinze, kutokana na majibu ya mthamini kiwango cha ardhi hakijafikia kulipwa 3800 kwa mita moja ya mraba, hivyo kinachostahili ni Sh. 1,200 kulingana na jiografia ya eneo ilivyo.

Mwenyekiti huyo aliwaomba wananchi hao kutia saini malipo ya fidia waliyoandaliwa na wakati hoja zao zinashughulikiwa ili shughuli za mradi ziendelee.

# Mabasi yazuiwa kusafirisha abiria kwa sababu mabovu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani, kimekamata mabasi matano kati ya 30 na kuyazuia kuendelea na usafirishaji wa abiria katika kituo kikubwa cha mabasi mjini Kahama baada ya kuwa na makosa makubwa, hivyo kuhatarisha maisha ya abiria.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika kituo hicho wakati wa ukaguzi wa magari hiyo, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Shinyanga, Mrakibu (SP) Malege Kilakala, alisema pamoja na kukagua mabasi hayo, pia wanatoa elimu mbalimbali kwa abiria kuhusu usalama wao wanapokuwa wakisafiri.

Kilakala alisema wamekagua mabasi yote yanayokwenda mikoani na kubaini mabasi 30 yakiwa na makosa mbalimbali na kuyapiga faini na kuyaacha kuendelea na safari huku mabasi matano yakizuiwa baada ya kubainika kuwa na makosa makobwa yanayoweza kuhatarisha usalama wa abiria.

"Ukaguzi katika kituo hiki umebaini magari mengi ni mabovu na yanahitaji kufanyiwa marekebisho madogo. Magari ambayo yalikuwa na matatizo ya kawaida tumeyapiga faini na kuyaacha kuendelea na safari na yale mabovu zaidi tumesitisha safari," alisema.

Alisema mabasi hayo yamekutwa na makosa makubwa yakiwamo kuisha kwa matairi na breki kutokufanya kazi vyema jambo ambalo ni hatari kwa maisha ya abiria huku akisisitiza kuwa ni vyema abiria wakachelewa kufika wanakokwenda kuliko kupanda magari mbaovu.

Kilakala alisema lengo la ukaguzi huo ni kuangalia usalama wa abiria wawapo safarini ikiwa ni pamoja na kuangalia matendo ambayo yanakwenda kinyume cha kanuni za usalama barabarani na kuchukua hatua kwa madereva wanaovunja sheria.

Mkuu huyo aliwataka wamiliki wa mabasi kuhakikisha magari yao yanakuwa na ubora unahitajika kabla ya kuingia barabarani kwa kuangalia mifumo ya taa, bodi na injini kama vinafanya kazi vyema na kwamba suala hilo litakuwa endelevu.

Johnson Kayambo, aliyekuwa akisafiri kutoka Kahama kwenda Kigoma, alisema mabasi mengi yanayobeba abiria ni mabovu, hivyo ukaguzi huo unaweza kuwafanya hata abiria kuwa na imani na magari wanalosafiria kwa kuwa litakuwa limekaguliwa na mamlaka husika.

Naye Elizabetha Josephat alisema ukaguzi huo ni muhimu na ni bora ukawa endelevu kwa kuwa hakuna abiria ambaye hapendi kufika salama mahali anakokwenda lakini ni vigumu kutambua basi lipi ni nzima na lipi ni bovu.

# TAWA yatenga bil. 1.6/- maendeleo kuendeleza pori la akiba

**Na Christina Haule,** NJOMBE

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) imetenga Sh. Bilioni 1.57 kwa ajili ya uendelezaji na usimamizi wa pori la akiba la Mpanga-kipengere wilayani Wanging'ombe mkoani hapa.

Fedha hizo ambazo zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2021/22, zitatumika kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo kuboresha utalii na kufanya watalii kuongezeka kutoka 7,000 hadi kufikia 100,000 kwa mwaka.

Akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea pori hilo, Mhifadhi Mwandamizi kutoka TAWA Mpanga-Kipengere, Alfred Kipondamali, alisema fedha hizo zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kitalii katika maeneo ya kiimani itakayogharimu Sh. milioni 90 sambamba na kuboresha maisha ya watumishi katika pori hilo.

Kipondamali ambaye pia ni Kaimu Kamanda wa Pori la Akiba Mpanga-Kipengere, alisema ujenzi huo utahusisha ujenzi wa 'Campsite' yenye thamani ya Sh. milioni 120, ujenzi wa daraja lenye thamani ya Sh. milioni 70 litakalowezesha watalii kutoka maeneo ya kimani kwenda Ikovu na kuondoa adha ya ukosefu wa barabara ya uhakika ya kuingia hifadhini.

Alitaja vingine kuwa ni ujenzi wa geti la watalii lenye thamani ya Sh. milioni 200, ujenzi wa nyumba ya watumishi yenye thamani ya Sh. milioni 102 sambamba na ujenzi wa barabara unaoendelea kwa sasa wenye thamani ya Sh. milioni 180 unaofanywa na kampuni ya SUMA JKT.

"Awali watalii walikuwa wakifika na kulala kwenye mahema ambapo kwa sasa ujenzi huu utasaidia kuwa na mahali pa kulala, kupumzika na kuongeza thamani ya utalii katika pori hili," alisema Kipondamali.

Kipondamali alisema pori hilo lilianzishwa mwaka 2002 likiwa na ukubwa wa kilometa za mraba 1,524 likiwa ndani ya mikoa ya Mbeya kwenye wilaya ya Mbarali na Njombe kwenye wilaya za Wanging'ombe na Makete.

Alitaja malengo ya kuanzishwa pori hilo ni kutunza hifadhi ya vyanzo vya maji ambapo pori hilo linachangia zaidi ya asilimia 40 ya maji yanayoenda kwenye mabwawa makubwa ya kutengeneza umeme ya kidatu na Mtera sambamba na Bwawa na Mwalimu Nyerere.

TAWA ina mapori ya akiba zaidi ya 20 ambayo huyatumia katika kutangaza vivutio vya utalii ikiwemo wanyama, misitu na safu za milima zilizojaa maua.

# Vijana 20 Kitanzania kushiriki mkutano Ufaransa

**Na Salome Kitomari**

WATANZANIA vijana 20 kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali na binafsi nchini yanayojishughulisha kuhudumia jamii, wanatarajia kushiriki mkutano wa kimataifa wa uhusiano baina ya Ufaransa na Afrika.

Akizungumza jana na waandishi wa habari katika ofisi za Ubalozi, Dar es Salaam, Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui, alisema mkutano huo utafanyika katika mji wa Montpellier Oktoba 8, mwaka huu, na utafunguliwa na kuhudhuriwa na Rais wa nchi hiyo, Emmanuel Macron.

Balozi Hajlaoui alisema mkutano huo utawaleta pamoja mamia ya waafrika wakiwamo wanaofanya sanaa, watetezi wa haki za binadamu, wanaharakati wa mazingira, watafiti, michezo, wajasiriamali vijana, washawishi mtandaoni na kwenye jamii na waandishi wa habari.

"Mkutano huu una malengo ya kutoa changamoto na kutafsiri upya ushirikiano baina ya Ufaransa na Afrika, kwa kuwasikiliza vijana, kujibu maswali yao, mjadala wa pamoja unaoangalia kesho yao," alisema Balozi Hajlaoui.

Kwa mujibu wa Balozi huyo, mkutano huo utakuwa wa wazi na utarushwa mubashara na kwenye mitandao ya kijamii kwa lengo la kuwafikia watu wengi duniani, ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha na fursa mbalimbali duniani.

Balozi Hajlaoui alisema ubalozi huo nchini utakuwa na matukio mawili yakatayofanyika kabla ya mkutano huo chini ya kauli mbiu ya namna watu wanajipatia fedha kutokana na mawazo na jingine ubunifu na namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Matukio yote mawili yatawezesha Ufaransa kuimarisha ushirikiano wake na Tanzania, kubaini fursa na maeneo ya ushirikiano na wadau mbalimbali kwa siku zijazo," alisema.

Wakizungumza kwa niaba ya washiriki wengine, Mkurugenzi Mtendaji wa Msichana Initiative, Rebeca Gyumi na Mkurugenzi Mtendaji wa Bakhresa Group, Aziz Salim Salim, walisema mkutano huo utawakutanisha na wawekezaji mbalimbali wa Kifaransa.

Pia alisema kutakuwa na nafasi ya kujinadi shughuli wanazofanya, kupata ujuzi mpya ambao watawashirikisha Watanzania katika kuongeza thamani na kuchangia ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.



Balozi wa Ufaransa hapa nchini, Nabil Hajlaoul (wa pili kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana kuhusu mkutano utakaojumuisha nchi za Afrika na Ufaransa utakaojadili mabadiliko ya Tabia nchi utakaofanyika katika mji wa Montpellier nchini humo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TIRA yahamasisha mawakala kujiendeleza

**Na Romana Mallya**

KAMISHNA wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Mussa Juma, amewataka mawakala wa bima wajiendeleze, ili kuongeza ujuzi utakaowawezesha kutoa huduma bora kwa wananchi na kulipa kodi zinazowahusu.

Dk. Juma aliyasema hayo jana Dar es Salaam katika mafunzo ya siku mbili yaliyoandaliwa na Chama cha Mawakala wa Bima Tanzania na kuwakutanisha mawakala kutoka mikoa mbalimbali yenye lengo la kuwajengea uelewa maeneo tofauti.

Alisema kadri teknolojia inavyokua, kunakuwa na ushindani kwenye soko, hivyo kama zilivyo sekta zingine, wanapaswa kujiendeleza ili wasitupwe nje.

"Jambo lingine ninataka kuwakumbusha, huwezi kuwa wakala wa kila kitu, chagua maeneo unayoyaweza, itawasaidia kukuza biashara zenu," alishauri.

Pia aliwataka ambao hawajajiunga kwenye umoja huo kujiunga kwa kuwa inasaidia malengo yaliyowekwa na serikali kufikiwa kwa muda mwafaka.

Dk. Juma alisema serikali ilizindua mpango mkuu wa kuboresha sekta ya fedha nchini kwa kipindi cha miaka 10 kwa mwaka 2020-2030 na mpango wa miaka mitano kwa mwaka 2020-2025 na ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) imeweka mikakati inayotakiwa kufikiwa.

"Sekta ndogo ya bima ni miongoni mwa sekta ya fedha ambayo inatekeleza mipango hii ya serikali, moja ya malengo tuliyowekewa sekta ya bima ni kuhakikisha uelewa wa Watanzania kuhusu bima unafikia angalau asilimia 80 ndani ya miaka 10 na Watanzania ambao ni asilimia 50 wanakuwa na bima angalau moja wapo," alisema.

Pia alisema jambo lingine ni sekta hiyo kuwa na utaratibu mzuri wa kushughulikia malalamiko na kero za wateja wa bima na kuwa na bidhaa zinazokidhi mahitaji ya Watanzania kulingana na shughuli wanazofanya.

Awali, Mwenyekiti wa Chama cha Mawakala wa Bima Tanzania, Sayi Daud, aliiomba serikali iliangalie suala la malipo yanayolipwa na wakala kama dhamana benki ambapo kwa kampuni moja hutoa Sh. milioni mbili ambayo kila mwaka hupanda.

"Hii ni tatizo kwa mawakala wapya kwao kupata Sh. milioni mbili ambazo zinakwenda kukaa benki tu hazifanyiwi chochote shida.

"Tunachoomba ikiwezekana iondolewe ili mawakala wapya wasiwe na kikwazo hicho, mtu anatoka chuoni anasajili kampuni yake bado anatakiwa atafute Sh. milioni mbili za kwenda kukaa benki tu hatakiwi kuzigusa," alisema.

# Halmashauri 5 kunufaika mradi wa kuzuia mdondoko wanafunzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI tano za wilaya nchini, zimetia saini makubaliano ya kutekeleza mradi wa kuondokana na tatizo la mdondoko kwa wanafunzi.

Halmashauri hizo ni Bahi, Chamwino, Ruangwa, Kilwa na Liwale ambazo zitatekeleza mradi huo wa majaribio na unasimamiwa na taasisi ya Price Water Coopers (PWC) kwa ufadhili wa Dola za Marekani 500,000 kutoka Shirika la Kimataifa la Korea (KOICA).

Akizungumza jana kuhusu mradi huo, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe, alisema halmashauri 20 zilishiriki kuandaa andiko la mradi huo lakini baada ya kuchambua maandiko hayo, zilichaguliwa halmashauri hizo tano.

Prof. Shemdoe alisema mradi huo unalenga kubaini vikwazo vinavyosababisha wanafunzi wengi kutomaliza masomo na kutafutia ufumbuzi.

"Niwapongeze sana kwenye hatua hii ya awali ya kushinda kuwa miongoni mwa halmashauri tano zilizochaguliwa. Nawashukuru sana wenzetu wa KOICA ambao ni wadau wa maendeleo.

Bwana Kyucheol Eo ambaye ndiye Mkurugenzi Mkazi wa KOICA, amekuja kushuhudia kitendo hiki cha kusaini (kutia saini) makubaliano haya ya kutekeleza mradi huu," alisema.

Prof.Shemdoe alishukuru KOICA kwa kusaidia Tanzania kwenye sekta ya elimu kwa watoto walioko shule ya msingi na sekondari ambao wanapata vikwazo na kusababisha kutofikia mwisho wa masomo yao.

"Kama ni shule ya msingi wanakwenda kabla ya kufikia darasa la saba wanaanguka njiani. Kuna changamoto (matatizo) nyingi (mengi), wengine wanapata mimba wakiwa njiani huko lakini wengine wanakuwa na sababu ambazo hazielezeki," alisema.

"Hivyo hivyo kwa wanafunzi wanaoanza kidato cha kwanza kwa mfano mwakani, tunategemea kuwa na wanafunzi milioni moja, hivyo tunatarajia baada ya miaka minne tuwaone wanamaliza kidato cha nne, lakini kwa bahati mbaya hapo njiani wakadondoka," alisema.

Alisema lengo ni kupunguza mdondoko kwa wanafunzi.

"Kwa niaba ya serikali kama wasimamizi wakuu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Elimu kwenye mamlaka hizi, kwa niaba ya Wizara ya Elimu (Sayansi na Teknolojia) tunapenda kuwahakikishia KOICA, PWC ushirikiano na kama kuna kitu mtahitaji msaada ofisi ipo wazi,"alisema.

Naye Kyucheol Eo, alisema miongoni mwa matatizo ya mdondoko ni wanafunzi kutembea umbali mrefu.

"Tanzania imefanya jitihada mbalimbali na kuongeza udahili wa wanafunzi, tutaendelea kuwa nanyi kwenye utekelezaji wa mradi wa EP4R, kuna mradi EPOSA ambao Januari 2022 baadhi ya halmashauri zitanufaika na mradi huu,"alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa PWC, Nelson Msuya, alisema wao wamepokea fedha na kupeleka kwenye Halmashauri hizo ili mipango yao itekelezwe inavyotakiwa.



Sheikh Ibrahim Kadura (kushoto) na Sheikh Hussein Jumbe (wa tatu kushoto), kutoka Kata ya Chang'ombe, jijini Dodoma, wakikagua maendeleo ya ujenzi wa msikiti wa Muccadam jana, unaojengwa kwa nguvu za waumini. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ndumbaro ahimiza uzalendo utumishi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Dk. Laurean Ndumbaro, amewataka watumishi wa umma kuwa wazalendo, waadilifu na weledi ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Dk. Ndumbaro aliyasema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akifungua kikao kazi cha siku mbili cha taasisi simamizi za maadili na vyama vya kitaaluma chenye lengo la kubadilishana uzoefu wa usimamizi wa maadili.

Alisema uzalendo, uadilifu na utendaji kazi unaozingatia weledi ndio nguzo kuu ya utendaji kazi wa watumishi wa umma ikiwa ni pamoja na ustawi wa taifa.

Alibainisha kuwa ofisi yake imekuwa na utamaduni endelevu wa kushirikiana na taasisi zinazosimamia maadili na vyama vya kitaaluma ili kujenga taifa imara lenye watumishi wa umma wazalendo na waadilifu.

"Ushirikiano uliopo kati ya ofisi yangu na taasisi simamizi za maadili na vyama vya kitaaluma, utasaidia kujenga uadilifu kwenye utumishi wa umma na jamii kwa ujumla," alisema Dk. Ndumbaro.

Alisema watumishi wa umma nchini wanao wajibu wa kuunga mkono kwa vitendo azma ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuujenga utumishi wa umma kuwa wenye kuzingatia uadilifu, uwajibikaji, kanuni, sheria, taratibu na miongozo iliyopo.

Mkurugenzi wa Ukuzaji Maadili, Ofisi ya Rais-Utumishi, Leila Mavika, alisema lengo kuu la kikao kazi hicho ni kukumbushana uzingatiaji wa maadili, kujadili changamoto za usimamizi wa maadili katika Utumishi wa Umma na kuzitafutia ufumbuzi.

Mwanasheria wa Bodi ya Wataalamu ya Ununuzi na Ugavi, Suleiman Mzava, ambaye ni mmoja wa washiriki wa kikao kazi hicho alisema, kikao kazi hicho kitasaidia kujenga uadilifu miongoni mwa taasisi za umma na kupongeza serikali kwa kuweka nguvu kubwa katika usimamizi wa maadili.

# Mkataba ujenzi ofisi za TAMISEMI watiwa saini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imetia saini mkataba na vikosi vya ujenzi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa ajili ya ujenzi wa jengo lake la ghorofa sita lenye thamani ya Sh. bilioni 23.5 katika Mji wa Serikali Mtumba jijini hapa.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alilolitoa Septemba 8, mwaka huu, la kuzitaka wizara zote 24 zikamilishe taratibu za ujenzi wa awamu ya pili ifikapo Septemba, 30, mwaka huu.

Akizungumza juzi baada ya kusaini mkataba huo, Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Prof. Riziki Shemdoe, alisema kazi hiyo itafanyika kwa miezi 24 kuanzia jana.

Prof. Shemdoe alimtaka mkandarasi wa ujenzi wa jengo hilo kuhakikisha linakuwa na ubora na thamani ya fedha inaonekana.

"Tayari tumeshawabidhi eneo la ujenzi, hii ni kazi ya miezi 24 ambayo inaanzia Oktoba mosi(jana) tunaamini baada ya kipindi hicho tutahama kutoka humu kwenda kwenye jengo letu la ghorofa sita, fedha hii ni kodi za wananchi hivyo tunataka tuone thamani ya fedha," alisema.

"Kama mwongozo unasema chumba cha Katibu Mkuu kiwe hivi ni lazima kiwe hivyo na value for money iwepo, tunataka majengo haya yadumu, mbona majengo ya mkoloni yalidumu muda mrefu," aliongeza.

Alisema jengo hilo la ghorofa sita litajengwa katika mji huo kwenye eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 29,000.

Alibainisha kuwa vikosi vilishinda zabuni ya ujenzi huku Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ni mshauri kwenye ujenzi huo.

Alisema kazi hiyo iliombwa na watu wanne ambao ni vikosi vya ujenzi, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), SUMA JKT na Mzinga Corporation lakini aliyefanikiwa kuipata kazi hiyo ni vikosi vya ujenzi.

Katika kutimiza azma ya serikali kuhamia Dodoma, serikali imepanga kutumia zaidi ya Sh. bilioni 600 kwa ajili ya kujenga awamu ya pili ya ujenzi wa majengo hayo.

Katika awamu ya kwanza serikali ilitumia Sh. bilioni 39 na majengo yamekamilika na kutumika huku zaidi ya watumishi 18,000 wameshahamia Dodoma.





# Msongamano darasani waathiri afya wanafunzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

IDADI kubwa ya wanafunzi darasani katika Shule ya Msingi Mtopepo imesababisha baadhi yao kupata matatizo ya viungo kutokana na kukosa nafasi.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana, wanafunzi wa shule hiyo walisema kutokana na idadi kubwa darasani, wanafunzi hawana hata nafasi ya kunyoosha miguu. Hali hiyo, walisema imesababisha baadhi ya viungo vyao vya mwili ikiwamo miguu kuuma na kufa ganzi.

Asha Seif, mmoja wa wanafunzi hao, alisema darasa analosoma halina madawati hivyo wanakaa sakafuni na kwamba hali waliyonayo ni hatarishi kwa sababu hakuna hata nafasi ya kunyoosha miguu.

"Hivi unavyotuona tumekaa ni hivi hivi hadi muda wa kutoka shule. Hatuna nafasi hata ya kunyoosha miguu tukiwa tumekaa. Mafuti yote yanatuuma," alisema mwanafunzi huyo.

Kutokana na hali hiyo, aliiomba serikali kutatua tatizo la uchache wa madarasa shuleni ili kuondokana na mrundikano mkubwa wa wanafunzi hali ambayo inachangia pia ufaulu mdogo.

Naye mwalimu wa shule hiyo ambaye hakutaka kutajwa jina lake, alikiri kuwapo kwa idadi kubwa ya wanafunzi darasani na tatizo hilo wameshaliwasilisha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Alisema shule hiyo ya msingi ina wanafunzi 4,065 na ina madarasa 24 na kwamba kati ya wanafunzi hao wasichana ni 2,079 na wavulana ni 1,986. Alisema darasa moja moja lina wastani wa wanafunzi 180. Kwa kawaida chumba kimoja cha darasa kinatakiwa kuwa na wastani wa wanafunzi 45.

Kwa mujibu wa mwalimu huyo. kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi madarasani, imewalazimu walimu wawili kufundisha darasa moja kwa wakati mmoja na kwamba mwalimu mmoja anafundisha na mwingine anasimamia utulivu wa wanafunzi.

"Ni kweli hali ni mbaya darasani wanafunzi wamejazana sana. Baadhi ya wanafunzi miguu inakufa ganzi kutokana na kukaa bila ya kupata nafasi ya kunyoosha mguu," alisema mwalimu huyo.

Pia alisema licha ya tatizo hilo la uchache wa madarasa, pia wana uhaba wa matundu ya vyoo shuleni hapo. Alisema vilivyopo havikidhi mahitaji.

Alisema vyoo vinavyotumika ni vinne kwa wanafunzi wa kiume 1,986 na vyoo viwili kwa wanafunzi 2,079 wa kike na kwamba vyoo hivyo vimeshajaa hali ambayo inahatarisha afya za wanafunzi.

"Hali kwa kweli hairidhishi shuleni hapa. Vyoo vimeshajaa na hili tumeshaliwasilisha wizara ya elimu lakini bado halijapatiwa ufumbuzi," alisema.

Akizungumza katika ziara yake Kisiwani Pemba mwanzoni mwa mwezi uliopita, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, alikiri kuwapo kwa uhaba wa madarasa pamoja na vyoo.

Dk. Mwinyi alisema hali hiyo imesababisha kuwapo kwa idadi kubwa ya wanafunzi madarasani na kuahidi kuwa serikali inatarajia kujenga madarasa 300 pamoja na vyoo kwa shule za unguja na Pemba ili kupunguza tatizo hilo.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Mtopepo, wakiwa wamesongamana darasani shuleni hapo, Wilaya ya Magharibi A, Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja jana, kutokana upungufu wa madarasa ambapo darasa moja lina wanafunzi 180. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mwinyi amshukuru Blair kusaidia SMZ

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, juzi alikutana na kufanya mazungumzo na Waziri Mkuu wa zamani wa Uingereza, Tony Blair, Ikulu Zanzibar.

Rais Dk. Mwinyi katika mazungumzo hayo, alishumkuru Blair kwa ujio wake wa mara ya pili Zanzibar katika mwendelezo wa ushirikiano baina ya Taasisi ya Mabadiliko Ulimwenguni (Tony Blair Institute for Global Change) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema taasisi hiyo itakuwa na jukumu la kuisadia serikali katika kubadilisha mifumo na kuhakikisha sera na mipango ya serikali inafanyika kwa vitendo, uwezeshaji kiuchumi na kuwajengea uwezo watendaji wa serikali.

Rais Mwinyi alisema maeneo muhimu ambayo taasisi ya Tony Blair itawekeza nguvu ni pamoja na sekta za uchumi wa bluu zikiwamo utalii, mafuta na gesi baharini, bandari na uvuvi.

Alisema wataalamu wa taasisi hiyo pia wataisaidia serikali katika sekta za kijamii zikiwemo elimu, maji, barabara, umeme na uwezeshaji wa ajira kwa jamii.

"Hatuna shaka kupitia uzoefu wake tutafanikiwa ikiwa tutafuata miongozo na maelekezo ya wataalam wao watakavyotuelekeza," alisema Dk. Mwinyi.

Naye Tony Blair alisema taasisi yake imefurahishwa na kuridhishwa na kazi inayofanywa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya uongozi wa Dk. Mwinyi na iko tayari kushirikiana nayo katika kuboresha mifumo na kujenga taasisi imara.

## Mama Mwinyi abainisha umuhimu Wiki ya UWT

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi, amesema Maadhimisho ya Wiki ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), yatawezesha kutambua na kutathmini mchango, maendeleo ya umoja huo na nafasi ya wanawake katika ujenzi na uimarishaji wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), serikali na jamii kwa jumla.

Mama Mwinyi ameyasema hayo jana katika hotuba yake aliyoitoa ya maadhimisho ya Wiki ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) 2021 kwa Wilaya ya Mjini, yaliyofanyika katika ukumbi wa Shule ya Chekechea Miembeni, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema mkusanyiko wa pamoja kati ya viongozi wa UWT na jumuiya zingine za CCM, viongozi wa serikali na wanachama wa CCM una maana ya kusherehekea na kutathmini maendeleo yanayoendelea kupatikana katika nyanja mbalimbali nchini.

Alielezea alivyovutiwa na madarasa ya ujasiriamali yaliyoko katika eneo hilo ambayo yameanzishwa kwa ajili ya kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vijana wa kike na wakiume ambao hawakubahatika kuendelea na elimu ya sekondari pamoja na wale wasioweza kujikimu kimaisha, wakiwamo wajane wenye kipato kidogo.

Alisema juhudi za UWT katika kuimarisha elimu ya ujasiriamali zinaenda sambamba na dhamira ya serikali ya Zanzibar na CCM ya kutoa nafasi za ajira 300,000 ifikapo mwaka 2025.

Mke huyo wa Rais alisema juhudi zinazochukuliwa na UWT katika kuimarisha chuo hicho na shughuli za ujasiriamali lazima zizingatie mambo matatu muhimu ambayo yamekuwa yakisisitizwa na Rais wa Zanzibar. Aliyataja mambo hayo kuwa ni elimu, mitaji na masoko.

Serikali, alisema hivi sasa inakamilisha taratibu za kuunganisha mifuko yote ya ujasiriamali kuwa mfuko mmoja imara ikiwa na lengo la kuhakikisha panakuwa na mfuko mmoja wenye nguvu na uwezo wa kutoa mikopo nafuu kwa vikundi mbalimbali ya wajasiriamali.

Katika hatua nyingine, Mama Mwinyi alisema kuna haja ya kuwakinga watoto wa kike na tatizo la mimba za utotoni ambazo huathiri elimu na mwelekeo mzima wa maisha yao.

Pia aliwataka wazazi na walezi kuwatunza na kuwalinda watoto na unyanyasaji wa kijinisia na kuwa wajasiri katika kutoa taarifa kwa serikali.



## MWANA FA

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI OKTOBA 2, 2021



MACHOZI YATAKUTOKA

# Ukisikia yaliyomtia hatiani R. Kelly

NI dhahiri mwimbaji mahiri wa Marekani, R. Kelly, anatarajiwa kupewa adhabu kali baada ya kukutwa na hatia ya unyanyasaji wa kingono na ubakaji.

Zaidi ya wiki tano, dazeni ya waathirika wa R. Kelly walisimama mahakamani kutoa ushahidi wao kuhusu vitendo vya unyanyasaji walivyofanyiwa ya mwimbaji huyo maarufu.

Kutokana na ushahidi wao, wengi wanatarajia kuona mbabe huyo wa muziki anapewa adhabu ya kifungo cha jela wakati hukumu yake itakapotolewa Mei 4, mwakani.

Jumla ya mashahidi 11, wakiwamo wanawake waliokumbana na unyanyasaji huo walitoa maelezo yao, huku wakimuelezea msanii huyo ni mtu mbabe, mwenye hasira na vurugu na kuongeza aliwataka wamuite "baba".

NINI ALIKIFANYA?

Shahidi mmoja aliyetambulishwa katika kesi hiyo Jane Doe, amesema alimnyanyasa kingono tangu akiwa na miaka 17 mwaka 2015 na pia aliambukizwa ugonjwa za zinaa unaoitwa herpes, ambao uliharibu ngozi.

Anasema R. Kelly hakumfahamisha kama alikuwa na ugonjwa huo kama sheria inavyotaka afanye.

"Mtu huyu alikusudia kabisa kuniambukiza ugonjwa alioujua," alisema.

Daktari wa Kelly baadae alitoa ushahidi wake kwamba muimbaji huyo alikuwa kwenye matibabu ya ugonjwa huo wa zinaa tangu 2007.

Mwanamke mwingine aliyetambulishwa kama Faith, ameiambia mahakama kwamba aliambukizwa na Kelly ugonjwa huo wa zinaa na mwanamke wa tatu aliyetambulishwa kama Kate, alithibitisha kupokea dola 200,000 kutoka kwa Kelly kama kumpooza na kumaliza mzozo baada ya kumlalamikia kuambukizwa virusi vya ugonjwa huo.

Jane amesema Kelly alijaribu kumdhibiti na kuna wakati alimpiga mpaka kumtoa makovu.

"Nilikuwa naadhibiwa vikali karibu kila baada ya siku mbili au tatu," mwanamke huyo ameiambia mahakama.

Shahidi Jerhonda Johnson Pace, ameiambia mahakama kwamba R. Kelly alijua kwamba alikuwa na umri mdogo mwaka 2009, pale walipofanya mapenzi huko Chicago, wakati huo alikuwa na umri wa miaka 17.

Mwanamke huyo mwenye miaka 28, alitoa ushahidi wake katika siku ya kwanza ya kesi hiyo akisema awali alimwambia R Kelly kwamba alikuwa na miaka 19, lakini hakuonekana kujali.

"Alinitaka nitengeneze nywele zangu na kuvaa kama binti skauti," amesema.

Mmoja wa watu hao akitumia jina la Louis, alisema alikutana kwa mara ya kwanza na Kelly mwaka 2006, wakati huo akiwa na umri wa miaka 17 akifanya kazi ya zamu ya usiku huko McDonald, Chicago.

"Akanambia iwe siri kati yangu na yeye kwani tumekuwa familia sasa, ni ndugu".

BASI SAWA

## Chameleone kuja kivingine

MASHABIKI wa mwanamuziki kutoka Uganda, Jose Chameleone, sasa wameanza kupata furaha baada ya msanii huyo kutangaza yupo sawa kiafya na anaweza kufanya kazi.

Chameleone ambaye alikabiliwa na matatizo ya ini na Kongosho hadi kupelekea kulazwa hospitalini, amedokeza anakuja na ujio wa wimbo wake wa kwanza 'Forever'.

Amesema ngoma hiyo amepanga kuitoa Oktoba 9, mwaka huu siku ya kuadhimisha Uhuru wa nchini hiyo.



## Cheed aanza safari rasmi Konde Gang

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Cheed kutoka lebo ya Konde Gang, amerusha kete yake ya kwanza tangu aondoke kwa Ali Kiba.

Cheed ametumia siku zaidi ya 350, kuachia ngoma yake mpya 'Wandia' ambayo kimsingi ndio itakayomfanya kuwa katika ushindani na wanamuziki wenzake chipukizi kama Ibrah na Tommy Flavour.

Kwenye wimbo huo mpya Cheed ameimba msichana wa Kibantu aliyempenda kijana mwenye maisha duni bila kujali wanapitia changamoto gani.





## Mwana FA yuko 'bize' msimpigie muziki

MBUNGE wa Muheza, Hamis Mwinjuma, maarufu kama MwanaFA, amesema kwa sasa wamuache awatumikie wananchi wake, licha ya muziki kuwa katika damu yake.

Akizungumza kwenye kipindi cha SupaBreakfast cha East Africa Radio, Mwana FA amesema kutokana na majukumu aliyonayo, inafikia hatua anakosa hata muda wa kufanya mazoezi ili kuweka viungo vya mwili wake sawa.

"Suala la muziki kwa sasa kusema ukweli Mungu atusaidie tutaona namna itakavyokuwa kama tutaweza kufanya tutafanya, lakini ngoja tuwatumikie wananchi wa Muheza kwanza," amesema MwanaFA

## Kijumbe: Pesa za mchezo haziliwi kama pipi

**Na Adam Fungamwango**

UTAMU ya filamu hii, pamoja na mafunzo kwenye jamii, lakini ni kumuangalia Riyama Ally, akipambana na Bi Hindu kwenye vita ya maneno. Hawa wote wanajulikana. Ni watu wenye maneno ya karaha na shombo. Ni watu wa vijembe. Hapa sasa wamekutana. Muongozaji na mtunzi wa filamu hawakutaka wacheze kama marafiki. Walijua ili picha linoge ni lazima wakwaruzane.

Filamu hii ya 'Kijumbe' ina ujumbe kuwa unaweza kufanya kitu ukadhani unamkomoa uliyemfanyika, kumbe athari zikarudi pia upande wako.

Kazembe, baada ya kujua kuwa dada yake Riyama anacheza upatu na kesho ni zamu yake ya kuchukua pesa, anakwenda kwa kijumbe ambaye ni Bi Hindi kumlaghai kuwa ametumwa na dada yake amchukulie pesa zake.

Bi.Hindu bila ya kujua hili wale lile, anamkabidhi Kazembe pesa kiasi cha shilingi laki moja na nusu. Kumbe sivyo alivyodhani. Kazembe anakwenda kutangaza ufalme kwenye baa. Riyama anatimba kwa kijumbe kudai pesa zake. Bi Hindu anamwambia alimpa kaka yake Kazembe. Hapo ndipo timbwili linapoanza. Kila mmoja anampachika mwenzake maneno ya shombo.

Riyama anakwenda kwa kaka yake kumuuliza. Kazembe anakataa. Mume wa Riyama anaye anataka pesa zake alizompa mkewe kwa ajili ya mchezo, kwa sababu aliambiwa kesho anakwenda kulipwa.

Pesa hazijapatikana, mume anatishia kumpa talaka mkewe. Zawadi, mpenzi wa Kazembe baada ya kupata taarifa nyingi kuhusu jambo hilo, anaamua kumsaidia kwa kuiba pesa shilingi laki moja na nusu nyumbani kwao ili deni lilipwe. Anampa mpenzi wake Kazembe akalipe, lakini kijana huyo anakwenda kuzitumia vibaya, kama alivyofanya zile za kwanza.

Bi Hindu anamshutumu Kazembe. Riyama anamdai Bi Hindu. Mume wa Riyama naye anaamua kumpa talaka moja mkewe kwa kutoona pesa za mchezo, Zawadi naye anampiga kibuti Kazembe kwa kosa la kutopeleka pesa ili deni lilipwe.

Hili linamfanya Kazembe kukosa raha kwani alilolifanya limemrudia yeye na dada yake Riyama ambaye amechwa na mumewe. Anaamua kuomba radhi. Anatafuta pesa. Anazipata laki na nusu na kumrudishia Bi. Hindu. Naye anamlipa Riyama. Anarudiana na mumewe. Kazembe anatafuta laki na nusu nyingine na kumpa Zawadi ili azirudishe kwao, na hapo uhusiano wao ukarejea.







## Nakaaya, Bexy wafanya 'Kitimtim' cha nguvu

MSANII wa Bongo Fleva, Bexy, amesema wakati wowote mashabiki wa muziki watamsikia upya Nakaaya Sumari, baada ya kimya cha muda mrefu.

Akizungumza na BT, Bexy amesema tayari wamerekodi wimbo mpya unaoitwa 'Kitimtim' na wakati wowote mashabiki watafurahia kuona video na audio ambayo itawatikisa vilivyo.

"Kama tunavyojua Nakaaya amekuwa kimya kwa muda mrefu, nashukuru kwa utayari wake wa kufanya kazi na mimi na kolabo yetu imekamilika itatoka muda wowote kutoka sasa hivyo mashabiki wakae tayari," amesema Bexy.

## NYIMBO HIZI HAZIPITWI NA WAKATI

**Na Adam Fungamwango**

WADAU wengi wa muziki wamekuwa wakiwashauri sana wasanii wa bongo fleva kuacha kutunga nyimbo za mapenzi kwa zaidi ya asilimia 90 na badala yake wajikite pia kutunga nyimbo za matukio.

Hata hivyo wamekuwa wakikumbana na upinzani mkali kwa vijana wa rika la sasa kuwa nyimbo za dansi na zile za zamani hazilipi na badala yake wasanii wengi wa sasa wamenufaika zaidi kiuchumi ni nyimbo hizi hizi ambazo wanaziponda.

Lakini ukweli utabaki pale pale kuwa nyimbo nyingi za kisasa, kwa sababu ni za mapenzi, huwa hazidumu muda mrefu zinasahaulika.

Kuna nyimbo zimepigwa zaidi ya miaka 50 iliyopita, lakini kwa sababu ni za matukio, hadi leo zimeendelea kupigwa linapokuja tukio au kumbukumbu ya tukio hilo.

Wanamuziki waliofanya hivyo huko nyuma, pamoja na kwamba baadhi yao wamefariki, lakini wamekuwa wakikumbukwa na kujulikana hadi leo na watakumbukwa vizazi na vizazi vijavyo.

Msanii gani hataki hili?

**1. Mkono wa Idd-Salum Abdallah**

Ni miaka zaidi ya 50 sasa imepita tangu kufariki kwa mwanamuziki maarufu, aliyekuwa staa miaka ya '50 hadi '60, Salum Abdallah. Ni zaidi ya miaka 60 imepita tangu aliporekodi kibao cha 'Mkono wa Idd'.

Alifariki mwaka 1965 mjini Morogoro kwa ajali ya gari, lakini wimbo wake huo umebaki kumbukumbu hadi kwenye kizazi cha leo, ambacho hakijapata kumshuhudia.

Kila mwaka inapokuja sikukuu ya Idd El Fitri, kibao hicho ndicho kinachopamba zaidi sikukuu hiyo kiasi hata kizazi cha leo hii kumfahamu. Kwa maana hiyo Salum ataendelea kukumbukwa vizazi kwa vizazi kutokana na wimbo huo tu ambao maudhui yale ni endelevu.

**2.Christmas-King Kiki**

Katikati ya miaka ya '70, mwanamuziki Kikumbi Mwanza Mpango, maarufu kama King Kiki, akiwa na bendi ya Maquiz Du Zaire alitunga kibao cha 'Christmas'. Ni wimbo ambao unazungumzia sikukuu ya Krismasi, ambapo Wakristo wote Duniani wanakumbuka kuzaliwa kwa Yesu Kristu zaidi ya miaka 2000 iliyopita. Ni wimbo ambao kila ikikaribia Desemba 25 ni lazima usikike. Kutokana na hali hiyo, Kiki ataendelea kukumbukwa na wimbo wake kupigwa vizazi kwa vizazi.

**3. Siku ya Kufa- Dk. Remmy Ongalla**

Mwanamuziki Dk. Remmy Ongalla, ni mmoja wa wasanii ambao hawatosahaulika na vizazi hadi vizazi kutokana na kutunga nyimbo kadhaa za matukio, hasa za vifo. Mwishoni mwa miaka ya '70, alitunga wimbo wa 'Siku ya Kufa' akiwa na Orchestra Makassy. Pamoja na mambo mengine, ni wimbo unaozungumzia binadamu anapofariki, anaacha ndugu, jamaa na pia haendi na mtu yoyote yule kaburini hata mke au mume.

Kutokana na kutokuwepo kwa nyimbo za vifo kwa kizazi cha sasa, ni wimbo unaotumika mno kwenye maombolezo, wanapofariki viongozi, mastaa, wanamuziki au watu muhimu kwenye jamii kila inapotokea.

**4. Noeli-King Kiki**

Huyo huyo mzee Kiki, mwanzoni mwa miaka ya '80 alipotoka Maquiz na kujiunga na Orchestra Safari Sound (OSS) iliyokuwa na mtindo wa Masantula, alitunga wimbo mwingine wa Krismasi, uitwao 'Noeli'.

Maudhui ni yale yale, kuizungumzia sikukuu hiyo, kitu ambacho kinamuweka kwenye orodha ya wasanii ambao kila mwaka ikikaribia sikukuu hiyo, sauti yake itasikika, kwani ni wimbo ambao ni lazima upigwe kwenye redio.

**5. Kifo-Dk. Remmy Ongalla**

Miaka ya '80, Dk. Remmy alirudi tena. Safari hii akiwa na Super Matimila, alitunga wimbo wa 'Kifo'.

Staili ya wimbo huu ni kama vile anakilalamikia kifo kuwa kwa nini kinaua watu. Kwa nini kimekuwa katili? Kinaua watu wote na hakichagui. Hata uwe bondia au mtemi vipi, siku ikifika utakwenda.

Ni wimbo ambao linapokuja suala la maombolezo ya kitaifa au kifo cha kiongozi, staa yoyote nchini, ni lazima utapigwa. Na kama zikikosekana nyimbo za aina hiyo kwa wasanii wa kisasa utaendelea kupigwa kizazi kwa kizazi. Remmy alifariki mwaka 2010 jijini Dar es Salaam.



# Tacha hata wewe una umbo bandia?

ALIYEKUWA mshiriki wa shindano la Big Brother Nigeria (BBNaija), Tacha, ameweka wazi kwamba amefanyiwa upasuaji wa kubadili mwili wake.

Tacha ambaye amejizolea mashabiki wengi, amesema hayo wakati akimjibu shabiki yake aliyemuuliza kama amefanyiwa upasuaji wa kubadili viungo vyake ili kuwa mrembo zaidi.

Kutokana na upasuaji huo, Tacha ameungana na wasanii wengine maarufu wa kike waliofanyiwa upasuaji kama Tonto Dikeh.



## Will Smith kumbe uko huru kuchepuka

MWIGIZAJI na mwanamuziki mkongwe wa Marekani, Will Smith, amezungumzia mambo yanayoendelea katika ndoa yake na mkewe Jada Pinkett, akisema uhusiano upo wazi.

Msanii huyo amekata kiu ya mashabiki wake ambao walikuwa wakipata fununu kuwa ndoa yao imefungwa kwa mkataba maalum ambao kila mmoja yupo huru kuwa na uhusiano na mtu mwingine.

Katika mahojiano na jarida maarufu la GQ , Smith, amesema ndoa sio gereza na kama watu wakikubaliana wapo huru kuwa na uhusiano na mtu mwingine huku akimjengea heshima mwenzake.


## Ndoa ya mastaa wakongwe yavunjika

MSHTUKO! Unaweza kusema hivyo baada ya mwanamuziki nyota wa Marekani, Miguel na mkewe Nazanin Mandi, kutangaza wameachana rasmi.

Wawili hao wameishi katika ndoa yao kwa muda wa miaka 17, walioana mwaka 2016, baada ya kuishi kama wachumba kwa zaidi ya miaka 10.

"Baada ya miaka 17 ya kuishi pamoja, Miguel na Nazanin Mandi wameamua kuachana na wapo hivyo kwa muda sasa. Kila mtu amemtakia heri ya anapoelekea," uliandika mtandao wa People.





## Kardi B wewe noma!

RAPA mkali kutoka Marekani, Cardi B, amewafurahisha mashabiki wake baada ya kuchapisha picha akionekana amevaa nguo zilizotengenezwa na mbuni wa kimataifa.

Mwanamuziki huyo ambaye ameshiriki maonyesho ya Wiki ya mavazi ya Paris, alikuwa kivutio kutokana na nguo alizovaa kumtoa vyema.

Cardi B, alionekana amevaa nguo zilizobuniwa na Manfred Thierry Mugler, ambaye ni maarufu katika taasnia ya mavazi Ulaya na Marekani.

## Regina utajengewa sanamu Lagos

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Regina Askia, sasa anakuwa miongoni mwa wasanii wa Nigeria wanaomiliki nyumba nchini Marekani.


Msanii huyo nyota wa filamu, ameweka wazi kupitia ukurasa wa Instagram kwamba amenunua nyumba nchini humo.


"Napenda kuwaarifu mwezi huu wa Septemba nimejifanyia mambo makubwa kwa kununua nyumba, namshukuru Mungu kwa kunifanyia mambo makubwa kwangu," ameandika Regina.



# Wafanyakazi majumbani walivyoathiriwa na janga la COVID-19 linaloendelea nchini

**Na Jenifer Gilla**




MIAKA mitatu iliyopita maisha ya Janet Michael (27), yalibadilika na kuwa bora wakati alipopata kazi kama mtumishi wa nyumbani jijini Dar es Salaam.

Janet ilimbidi kutembea karibu kilomita 1,365 kutoka nyumbani kwao Bukoba, hadi eneo la Tabata jijini Dar es Salaam.

Janet alijiona mwenye bahati kubwa kupata kazi hiyo ambayo ilimwingizia Sh. 50, 000 ambayo ilimsaidia kutunza watoto wake wawili na wazazi wake ambao ni wazeee.

Hata hivyo, mipango yote imekuwa bure tangu kutokea janga la Covid-19, kwani mwajiri wake alikuwa miongoni mwa walipoteza kazi zao kutokana na janga hilo.

"Sikuamini aliponipa Sh. 50, 000 na kuniambia huo ndio mshahara wa mwisho, niliishiwa nguvu. Hata hivyo, aliniambia kuwa kuanzia sasa atapunguza mshahara wangu hadi Sh.30, 000, nilipojaribu kupinga, aliniambia ninaweza kuacha kazi, "anasema Janet.

Akikabiliwa na chaguo la kukosa kazi na bila msaada wowote kwa watoto wake wawili, Janet aliendelea kufanya kazi kwa shingo upande huku akutafuta kazi sehemu.

Mwezi mmoja baadaye, Janet alibahatika kupata kazi sehemu nyingine ambapo mwajiri wake mpya aliahidi kumlipa kiasi cha Sh. 60,000.

Kazi mpya ilikuja na changamoto mpya, kwani hapo awali alifanya kazi katika familia ndogo, lakini huko ilikuwa tofauti, ilijumuisha kutunza familia ya watu sita, wakiwamo watoto wanne.

Huko alifanya kazi tangu alfajiri hadi usiku wa manane kutokana na familia nzima kuwapo nyumbani kipindi cha likizo ya Corona.

Mwishowe Janet aliugua na kwenda hospitali ambako aliambiwa anasumbuliwa na uchovu. Alishauriwa kupumzika, jambo ambalo halikuwezekana kwani alihatarisha kupoteza kazi!

Janet ni miongoni mwa wafanyakazi wa nyumbani 1,087,401, ambao ni asilimia tano ya idadi ya wanaopambana na changamoto zilizoongezeka zinazosababishwa na janga la COVID-19.

Wafanyakazi wengi wa nyumbani ni wanawake ambao mishahara yao ilipunguzwa wakati wa kipindi cha likizo ya corona na wengine kuachishwa kazi.

Utafiti wa wafanyakazi wa nyumbani katika nchi 14 za Kiafrika uliofanywa na Shirikisho la Kimataifa la Wafanyakazi wa Nyumbani (IFDW), unaonyesha kuwa asilimia 85 ya wafanyakazi wa nyumbani ambao walifutwa kazi, hawakupata malipo ya kuachishwa kazi.

Wale ambao walibakiza kazi zao wamepunguzwa mapato yao ambayo yamekuwa na athari kubwa kwa kaya zao.

Kutokana na hali halisi ya mazingira ya kazi, Janet na wengine kama yeye wako katika hatari kubwa ya kuambukizwa ugonjwa kutoka kwa kaya wanazofanya kazi, kwa kuwa wanafanya kazi bila ya kuwa na vifaa vya kujikinga na virusi hivyo.

Kulingana na utafiti huo, asilimia 53 ya wafanyakazi wa nyumbani hawana fursa ya kulipwa siku za wagonjwa ambazo zinaongeza hatari ya kuambukizwa na kudhoofisha uwezo wao wa kujitunza wenyewe na familia zao.

Hiki ndicho kilichotokea kwa Mary Michael (18), mfanyakazi mwingine wa nyumbani kutoka Masaki.

Wakati Mary alipata virusi vya Corona, mwajiri wake alimrudisha kwenye Kituo cha kazi kinachotoa mafunzo na kusambaza wafanyakazi wa majumbani kiitwacho Quiz Cup Center.

"Bosi wangu pia alikuwa na dalili kama hizo.

Alipompeleka hospitalini alipimwa COVID-19 na kukutwa na maambukizi na sote tukapewa dawa.

Siku inayofuata mwajiri alinirudisha kwa wakala.

Nilijisikia vibaya sana, nilifikiri labda walinirudisha kwa sababu wanadhani mimi ndiye niliyewapa ugonjwa, "Mary anasema.

Kiwango cha juu cha kutothaminiwa wafanyakazi wa majumbani inamaanisha kuwa hawana usalama wa kazi na wana ulinzi mdogo.

Inakadiriwa kuwa asilimia 81 ya wafanyakazi wa nyumbani hawana mikataba iliyoandikwa na hufanya kazi kwa msingi wa makubaliano ya mdomo. Zaidi ya asilimia 60 ya wafanyakazi hawana usalama wa kijamii au bima ya matibabu.

Jenifer Mwavula, pia alipoteza kazi wakati alipopiga chafya mbele ya mwajiri wake. Tulimpata Jenifer kwa wakala wa ajira wa wafanyakazi wa nyumbani jijini Dar-es-Salaam ambapo alikuwa ameenda kutafuta nafasi nyingine.

"Sikuweza kutembelea familia yangu kwani niliruhusiwa kuondoka na mwajiri wangu ambaye aliogopa kwamba ikiwa ningesafiri ningerudi na virusi. Kwa pesa kidogo ambayo walikuwa wakinilipa, watoto wangu hawawezi kupata chakula cha kutosha" anasema Jenifer.

Mawakala huwalinda vipi wafanyakazi?

Wakala Eliwanjela Jamesa kutoka Quiz Cup Center, anasema alipokea malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi ambao wamekabiliwa na unyanyasaji mwingi kipindi cha likizo ya kupisha maambukizi ya corona ikiwamo kufanyishwa kazi kupita kiasi, kufukuzwa na kuvunjwa haki zao na waajiri ambao wanaogopa kuambukizwa.

Anasema hata mahitaji ya wafanyakazi yalipungua tangu janga hilo lilipoanza.

. "Hatukuwa na njia nyingine isipokuwa kuwaachilia wasichana warudi makwao, wengi wao kutoka vijijini, kwani uhitaji wa wasichana wa kazi ulipungua sana," alisema.

### Elimu

Margaret Tibaijuka, Meneja wa Precious Daywaka, anasema wamekuwa wakiwaelimisha wafanyakazi wa majumbani juu ya virusi vya corona na jinsi ya kujikinga kama vile kutumia vitakasa mikono, kuvaa glavu na barakoa, usafi wa kibinafsi na kuzingatia hatua zingine za msingi za usalama.

Kwa upande wa Veneranda Chisel, anaeleza ingawa alitaka kutoa msaada unaofaa kwa mfanyakazi wake wa nyumbani, lakini hakuwa na pesa ya kutosha kumpatia mfanyakazi huyo .

"Nimekuwa nje ya ajira kwa zaidi ya mwaka mmoja, ilibidi nimwachishe kazi mfanyakazi wangu wa nyumbazi kwani sikuwa na pesa ya kumlipa," Veneranda anasema.

### Tamko la serikali

Tofauti na nchi zingine ambazo zilichukua hatua za kuwalinda wafanyakazi wa ndani walio katika mazingira magumu, hapa nchini sheria inalenga zaidi wafanyakazi walio katika ajira rasmi na kupuuza wale walio katika sekta isiyo rasmi ambayo ni pamoja na wafanyakazi wa nyumbani.

Mkurugenzi wa Masuala ya Watoto katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Sebastian Kitiku, anasema idara yake haijapokea maombi yoyote ya usaidizi kwa wafanyakazi wa majumbani ingawa alikiri mambo haya yanafanyika mitaani na kuna haja ya kuwapo msaada kama huo katika jamii.

Mwenyekiti wa Chama cha wafanyakazi wa mahotelini, mshambani (CHODAWU) katika Wilaya za Ilala na Temeke, Wagala Chunga, anasema umoja huo umekuwa ukiwaelimisha wanachama wake juu ya viwango vya afya na usalama kazini, haki zao na majukumu ya mwajiri.

Anasema kuna haja ya serikali kuridhia Mkataba wa Wafanyakazi wa Majumbani Na 189 wa 2011, uliopitishwa na Shirika la Kazi Duniani (ILO).

"Kuwachanganya wafanyakazi wa nyumbani na wafanyakazi wengine si haki kwa sababu ya aina ya kazi yao, saa za kazi, ulinzi wa jamii na mazingira.

Kwa mfano, wengi wao huishi na kulala katika sehemu zao za kazi huku wakipata mshahara kati ya Sh. 30,000 na 150,000 , "Chunga anasema.


Shirika la kazi duniani (ILO) linakadiria kuna watumishi wa majumbani milioni 67 ulimwenguni huku milioni 17 ni watoto chini ya miaka 18 na milioni 7 ni chini ya miaka 15.


Shirika hilo linaelezea baadhi ya changamoto zinazopitia kundi hili kipindi hiki cha janga la virusi vya corona kuwa ni kukosa ajira, haki ya kukosa taarifa kuhusu afya ya uzazi, msongo wa mawazo na afya ya akili, kukosa chakula na malazi na unyanyasi na unyanyapaa sehemu ya kazi.

MAKALA

# Wafanyakazi majumbani walivyoathiriwa na janga la Covid-19 linaloendelea nchini

**Na Jenifer Gilla**




MIAKA mitatu iliyopita maisha ya Janet Michael (27), yalibadilika na kuwa bora wakati alipopata kazi kama mtumishi wa nyumbani jijini Dar es Salaam.

Janet ilimbidi kutembea karibu kilomita 1,365 kutoka nyumbani kwao Bukoba, hadi eneo la Tabata jijini Dar es Salaam.

Janet alijiona mwenye bahati kubwa kupata kazi hiyo ambayo ilimwingizia Sh. 50, 000 ambayo ilimsaidia kutunza watoto wake wawili na wazazi wake ambao ni wazeee.

Hata hivyo, mipango yote imekuwa bure tangu kutokea janga la Covid-19, kwani mwajiri wake alikuwa miongoni mwa walipoteza kazi zao kutokana na janga hilo.

"Sikuamini aliponipa Sh. 50, 000 na kuniambia huo ndio mshahara wa mwisho, niliishiwa nguvu. Hata hivyo, aliniambia kuwa kuanzia sasa atapunguza mshahara wangu hadi Sh.30, 000, nilipojaribu kupinga, aliniambia ninaweza kuacha kazi, "anasema Janet.

Akikabiliwa na chaguo la kukosa kazi na bila msaada wowote kwa watoto wake wawili, Janet aliendelea kufanya kazi kwa shingo upande huku akutafuta kazi sehemu.

Mwezi mmoja baadaye, Janet alibahatika kupata kazi sehemu nyingine ambapo mwajiri wake mpya aliahidi kumlipa kiasi cha Sh. 60,000.

Kazi mpya ilikuja na changamoto mpya, kwani hapo awali alifanya kazi katika familia ndogo, lakini huko ilikuwa tofauti, ilijumuisha kutunza familia ya watu sita, wakiwamo watoto wanne.

Huko alifanya kazi tangu alfajiri hadi usiku wa manane kutokana na familia nzima kuwapo nyumbani kipindi cha likizo ya Corona.

Mwishowe Janet aliugua na kwenda hospitali ambako aliambiwa anasumbuliwa na uchovu. Alishauriwa kupumzika, jambo ambalo halikuwezekana kwani alihatarisha kupoteza kazi!

Janet ni miongoni mwa wafanyakazi wa nyumbani 1,087,401, ambao ni asilimia tano ya idadi ya wanaopambana na changamoto zilizoongezeka zinazosababishwa na janga la COVID-19.

Wafanyakazi wengi wa nyumbani ni wanawake ambao mishahara yao ilipunguzwa wakati wa kipindi cha likizo ya corona na wengine kuachishwa kazi.

Utafiti wa wafanyakazi wa nyumbani katika nchi 14 za Kiafrika uliofanywa na Shirikisho la Kimataifa la Wafanyakazi wa Nyumbani (IFDW), unaonyesha kuwa asilimia 85 ya wafanyakazi wa nyumbani ambao walifutwa kazi, hawakupata malipo ya kuachishwa kazi.

Wale ambao walibakiza kazi zao wamepunguzwa mapato yao ambayo yamekuwa na athari kubwa kwa kaya zao.

Kutokana na hali halisi ya mazingira ya kazi, Janet na wengine kama yeye wako katika hatari kubwa ya kuambukizwa ugonjwa kutoka kwa kaya wanazofanya kazi, kwa kuwa wanafanya kazi bila ya kuwa na vifaa vya kujikinga na virusi hivyo.

Kulingana na utafiti huo, asilimia 53 ya wafanyakazi wa nyumbani hawana fursa ya kulipwa siku za wagonjwa ambazo zinaongeza hatari ya kuambukizwa na kudhoofisha uwezo wao wa kujitunza wenyewe na familia zao.

Hiki ndicho kilichotokea kwa Mary Michael (18), mfanyakazi mwingine wa nyumbani kutoka Masaki.

Wakati Mary alipata virusi vya Corona, mwajiri wake alimrudisha kwenye Kituo cha kazi kinachotoa mafunzo na kusambaza wafanyakazi wa majumbani kiitwacho Quiz Cup Center.

"Bosi wangu pia alikuwa na dalili kama hizo.

Aliponipeleka hospitalini alipimwa COVID-19 na kukutwa na maambukizi na sote tukapewa dawa.

Siku inayofuata mwajiri alinirudisha kwa wakala.

Nilijisikia vibaya sana, nilifikiri labda walinirudisha kwa sababu wanadhani mimi ndiye niliyewapa ugonjwa, "Mary anasema.

Kiwango cha juu cha kutothaminiwa wafanyakazi wa majumbani inamaanisha kuwa hawana usalama wa kazi na wana ulinzi mdogo.

Inakadiriwa kuwa asilimia 81 ya wafanyakazi wa nyumbani hawana mikataba iliyoandikwa na hufanya kazi kwa msingi wa makubaliano ya mdomo. Zaidi ya asilimia 60 ya wafanyakazi hawana usalama wa kijamii au bima ya matibabu.

Jenifer Mwavula, pia alipoteza kazi wakati alipopiga chafya mbele ya mwajiri wake. Tulimpata Jenifer kwa wakala wa ajira wa wafanyakazi wa nyumbani jijini Dar-es-Salaam ambapo alikuwa ameenda kutafuta nafasi nyingine.

"Sikuweza kutembelea familia yangu kwani niliruhusiwa kuondoka na mwajiri wangu ambaye aliogopa kwamba ikiwa ningesafiri ningerudi na virusi. Kwa pesa kidogo ambayo walikuwa wakinilipa, watoto wangu hawawezi kupata chakula cha kutosha" anasema Jenifer.

Mawakala huwalinda vipi wafanyakazi?

Wakala Eliwanjela Jamesa kutoka Quiz Cup Center, anasema alipokea malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi ambao wamekabiliwa na unyanyasaji mwingi kipindi cha likizo ya kupisha maambukizi ya corona ikiwamo kufanyishwa kazi kupita kiasi, kufukuzwa na kuvunjwa haki zao na waajiri ambao wanaogopa kuambukizwa.

Anasema hata mahitaji ya wafanyakazi yalipungua tangu janga hilo lilipoanza.

. "Hatukuwa na njia nyingine isipokuwa kuwaachilia wasichana warudi makwao, wengi wao kutoka vijijini, kwani uhitaji wa wasichana wa kazi ulipungua sana," alisema.

## Elimu

Margaret Tibaijuka, Meneja wa Precious Daywaka, anasema wamekuwa wakiwaelimisha wafanyakazi wa majumbani juu ya virusi vya corona na jinsi ya kujikinga kama vile kutumia vitakasa mikono, kuvaa glavu na barakoa, usafi wa kibinafsi na kuzingatia hatua zingine za msingi za usalama.

Kwa upande wa Veneranda Chisel, anaeleza ingawa alitaka kutoa msaada unaofaa kwa mfanyakazi wake wa nyumbani, lakini hakuwa na pesa ya kutosha kumpatia mfanyakazi huyo .

"Nimekuwa nje ya ajira kwa zaidi ya mwaka mmoja, ilibidi nimwachishe kazi mfanyakazi wangu wa nyumbazi kwani sikuwa na pesa ya kumlipa," Veneranda anasema.

## Tamko la serikali

Tofauti na nchi zingine ambazo zilichukua hatua za kuwalinda wafanyakazi wa ndani walio katika mazingira magumu, hapa nchini sheria inalenga zaidi wafanyakazi walio katika ajira rasmi na kupuuza wale walio katika sekta isiyo rasmi ambayo ni pamoja na wafanyakazi wa nyumbani.

Mkurugenzi wa Masuala ya Watoto katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Sebastian Kitiku, anasema idara yake haijapokea maombi yoyote ya usaidizi kwa wafanyakazi wa majumbani ingawa alikiri mambo haya yanafanyika mitaani na kuna haja ya kuwapo msaada kama huo katika jamii.

Mwenyekiti wa Chama cha wafanyakazi wa mahotelini, mshambani (CHODAWU) katika Wilaya za Ilala na Temeke, Wagala Chunga, anasema umoja huo umekuwa ukiwaelimisha wanachama wake juu ya viwango vya afya na usalama kazini, haki zao na majukumu ya mwajiri.

Anasema kuna haja ya serikali kuridhia Mkataba wa Wafanyakazi wa Majumbani Na 189 wa 2011, uliopitishwa na Shirika la Kazi Duniani (ILO).

"Kuwachanganya wafanyakazi wa nyumbani na wafanyakazi wengine si haki kwa sababu ya aina ya kazi yao, saa za kazi, ulinzi wa jamii na mazingira.

Kwa mfano, wengi wao huishi na kulala katika sehemu zao za kazi huku wakipata mshahara kati ya Sh. 30,000 na 150,000 , "Chunga anasema.

Shirika la kazi duniani (ILO) linakadiria kuna watumishi wa majumbani milioni 67 ulimwenguni huku milioni 17 ni watoto chini ya miaka 18 na milioni 7 ni chini ya miaka 15.

Shirika hilo linaelezea baadhi ya changamoto zinazopitia kundi hili kipindi hiki cha janga la virusi vya corona kuwa ni kukosa ajira, haki ya kukosa taarifa kuhusu afya ya uzazi, msongo wa mawazo na afya ya akili, kukosa chakula na malazi na unyanyasi na unyanyapaa sehemu ya kazi.

# WANAYOPITIA WENYE SELIMUNDU

## ●Unyanyapaa tatizo sugu linalowaumiza

Na Christina Mwakangale

TAKWIMU zinasema Tanzania ni miongoni mwa nchi nne zenye idadi kubwa za wagonjwa wa selimundu duniani.

Mataifa ambayo yanaongoza ni India, Nigeria na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Sababu kubwa ambazo zinachangia nchi hizo kuwa na watu wenye matatizo ya selimundu ni kuwapo kwa ugonjwa wa malaria.

Mtu akiwa na tatizo la selimundu ni baada ya seli nyekundu za damu kuwa na umbo lisilo la kawaida la butu ambazo zinazuia kuwepo kwa mtiririko mzuri wa damu kwenye mishipa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi zinazojishughulisha na Ugonjwa wa Selimundu Tanzania (TANSCDA), Dk. Deogratius Soka, anasema Tanzania inakabiliwa na tatizo hilo kutokana na kuwa katika eneo la kitropiki lenye ugonjwa wa malaria kwa wingi.

"Hawa watu wenye selimundu wana ufanisi wao wa chembe hai nyekundu za damu. Chembe hai zao zina upungufu wa oksijeni.

Kwa kawaida chembe hai nyekundu kwa binadamu hutakiwwa kuishi muda mrefu siku 90 hadi 120.

"Wenye selimundu, seli nyekundu za zinaishi siku 10 hadi 20, kwa hiyo huo ni utofauti wa mtu wa kawaida na wa selimundu," anasema Dk. Soka.

Anasema selimundu ni ugonjwa usioambukiza kama magonjwa mengine.

Dk. Soka, anaeleza ugonjwa huo unatokana kwa kurithi na umekaa kwenye kinasaba.

"Huwezi kuupata ugonjwa huu hata uongezewe damu ya mtu mwenye selimundu hautopata ugonjwa huu, sababu unakaa katika vinasaba," anasema Dk. Soka.

### TIBA SELIMUNDU

Akizungumzia matibabu yake, Soka anasema selimundu ina namna yake ya kuitibu, ikiwamo kumtibu mgonjwa kwa kubadilisha uloho au uboho kwa kubadili damu kutoka kwenye mifupa ukichukua uboho wa mtu ambaye hana selimundu na kuweka kwa mgonjwa.

Anasema mgonjwa wa selimundu huishiwa damu kila baada ya siku chache na iwapo ataongezewa damu kwa kupitia uboho ataweza kupona kabisa kutegemeana na matibabu yenyewe.

"Kutengeneza damu isiyo na selimundu inawezekana, ulianza tangu siku nyingi kwa nchi zilizoendelea kama Afrika Kusini," anasema.

Hata hivyo, Tanzania tayari imezindua mfumo hivi karibuni wa kupandikizwa uboho.

"Kama watu wanaumwa mara kwa mara, hao tutawafanyia matibabu ya kupandikiza ubohoo haraka kwa sababu ya kuokoa maisha yao." anasema

Dk. Soka anasema matumizi ya dawa kwa wagonjwa yanakuwa ya kila siku ili kutengeneza damu kwa wingi kwenye mwili.

Anasema tiba nyingine ni matumizi ya dawa za kusaidia kupunguza maumivu makali kwa mgonjwa.

"Muongozo wa matibabu tumepeleka katika hospitali zote, mkakati wa kwenda kufundisha wafanyakazi wa afya wa msingi, zahanati na vituo vya afya nchi nzima," anabainisha Dk. Soka.

Katika kuhakikisha wanaishi katika mazingira mazuri, watu wenye selimundu wanakuwa na masharti ya kuyafuata ikiwamo kutokula sana, kutovuta sigara na kutofanya kazi kwa muda mrefu ili kuepuka uchovu.

Sharti lingine watu wenye selimundu wanatakiwa wasikae kwenye baridi kali na kama wapo maeneo yenye hali ya hewa ya aina hiyo wanapaswa kuvaa nguo nzito zinazotengeneza joto.

Anashauri watu walio kwenye mahusiano na wanaotarajia kufunga ndoa, ni muhimu kuchukua vipimo ili kubaini iwapo wana magonjwa ambayo yanahusisha vinasaba ili kupunguza uwezo mkubwa kurithisha watoto wao.




Easter Gabriel (25), mjamzito na mgonjwa wa kwanza wa selimundu kupatiwa matibabu ya uboho hivi karibuni katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), ambaye amebadilishiwa chembe hai nyekundu za damu kwa kutumia mashine za kisasa (Spectra Otia). **PICHA ZOTE: MTANDAO**




Dk. Degratius Soka (kulia), akizungumza na waandishi wa habari.

Anasema vipimo vya kitabibu, hutoa picha ya hali ya afya za wahusika ikiwamo dalili za ugonjwa wa selimundu, akibainisha kwamba hapa nchini asilimia 15 hadi 20 ya Watanzania wana vinasaba vya selimundu.

"Hatufikirii kwamba kupima wakati wa kuoana ni kipindi kizuri sana, kwa sababu watu waliofikia hatua hiyo hawawezi kurudi nyuma," anaongeza Dk Sako.

Arafa Said, ambaye anaishi na selimundu, anasema ni muhimu kila mtu anayeishi na tatizo hilo kujiona kama shujaa na kujiamini.

Mwanamke huyo ambaye ni Rais wa Chama cha Wanaoishi na Selimundu Tanzania, anasema kuna unyanyapaa katika jamii kutokana na kukosa elimu sahihi ya tatizo hilo.

"Unatakiwa uishi kama watu wengine na ujikubali na kujua ugonjwa wako unahitaji nini, na unatakiwa uwe makini kwa kufanya mazoezi, kula chakula bora na dawa kwa wakati.

"Kwenye selimundu unyanyapaaji upo kwa sababu elimu haipo na kama elimu ingekuwepo basi watu wasingenyanyapaliwa na watu kubaki kudhani ni ugonjwa wa ajabu sana, na elimu ingepaswa iwafikie ili kuondoa hofu" anasema Arafa.

### TAKWIMU

Kuhusu hali ya ugonjwa huo, Dk. Soka anasema duniani watoto 300,000 huzaliwa kila mwaka na ugonjwa wa selimundu, wakati 11,000 hadi 12,000 kila mwaka huzaliwa Tanzania na ikishika nafasi ya nne.

Anasema hadi sasa nchini kuna watoto 300,000 wenye selimundu na kwamba huchangia vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano kwa asilimia 6.7.

### WIZARA

Kaimu Mkurugenzi wa Tiba Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Sarah Maongezi anasema watoto 100 waliopo chini ya umri wa miaka mitano, hufariki dunia kila mwaka kutokana na ugonjwa huo.

Anasema idadi kubwa ya wagonjwa wanatoka mikoa ya Kanda ya Ziwa, hata hivyo chanzo bado hakijajulikana.

Mratibu wa Selimundu kutoka wizara hiyo, Asteria Mpoto, anasema serikali inaendelea kutoa elimu kuhusu ugonjwa huo na kila kila ifikapo Septemba Mosi hadi 30 wanafanya maadhimisho.

HABARI KIMATAIFA

# Kanali Doumbouya rais mpya Guinea

**Conakry,** GUINEA

BAADA ya mapinduzi ya kijeshi mwezi uliopita kumuondoa aliyekuwa Rais wa Guinea Alpha Condé, Kiongozi wa kijeshi, Kanali Mamady Doumbouya ameapishwa kuwa rais wa mpito.

Sherehe ya kuapishwa kwake zimefanyika katika Ikulu ya rais na kuhudhuriwa na waalikwa pekee.

Kanali Doumbouya aliongoza mapinduzi yaliyomuondoa madarakani Rais Alpha Condé mapema mwezi uliopita.

Anatarajiwa kuunda serikali katika wiki chache zijazo.

Kiongozi huyo wa kijeshi aliye na miaka 41, atakuwa kiongozi wa pili wa Afrika mwenye umri mdogo kuongoza nchi, mdogo zaidi akiwa ni wa Mali Kanali Assimi Goïta, 38 ambaye aliongoza mapinduzi ya kumng'oa madarakani Rais Keïta.

Baada ya mapinduzi ya Guinea Kanali Doumbouya alisema askari wake wamechukua uongozi na walitaka kumaliza ufisadi, ukiukwaji wa haki za binadamu na usimamizi mbaya uliokithiri nchini humo.

Rais Condé alichaguliwa katika uchaguzi uliokumbwa na utata kuongoza kwa muhula wa tatu licha ya maandamano ya ghasia mwaka jana.

**BBC**

# Buhari kuondoa zuio la Twitter kwa sharti

**Lagos,** NIGERIA

RAIS wa Nigeria, Muhammadu Buhari, ameamuru kuondolewa kwa marufuku dhidi ya mtandao wa kijamii wa Twitter, ikiwa kampuni hiyo kubwa ya teknolojia itatimiza masharti.

Rais Buhari alisema Wanigeria wanaweza kuendelea kutumia mtandao huo, iwapo ni kwa ajili ya biashara na masuala muhimu pekee.

Katika hotuba yake ya kuadhimisha sikukuu ya uhuru wa nchi hiyo, alisema kamati maalum inajadiliana na Twitter kuhusu masuala kadhaa ya usalama wa kitaifa, ushuru wa haki na utatuzi wa mizozo.

Serikali ya Nigeria, ilipiga marufuku huduma za Twitter tangu Juni, mwaka huu, baada ya mtandao huo wa kijamii kufuta ujumbe wa rais Buhari wenye utata.

Marufuku hiyo ilikosolowa vikali na mashirika ya kutetea haki za binadamu na wanaharakati wa kutetea uhuru wa vyombo vya habari.

**BBC**

# KANU yamteua Gideon Moi kuwania urais 2022

**Nairobi,** KENYA

WAJUMBE wa Halmashauri Kuu ya chama cha KANU, wamemuidhinisha Gideon Moi, kugombea urais katika uchaguzi wa mwaka 2022.

Moi (57), ni mwanasiasa na mtoto wa hayati Daniel Arap Moi, aliyekuwa rais wa pili wa Kenya kwa miaka 24 kati ya mwaka 1978 na 2002.

Moi alieleza kwamba, iwapo atapata ridhaa ya raia wa Kenya kwenye uchaguzi ujao, ataongoza serikali inayowajumuisha wote na kupambana na ufisadi.

Kongamano hilo la kitaifa la wajumbe limemuidhinisha Seneta huyo wa Jimbo la Baringo, kugombea urais kumrithi Rais Uhuru Kenyatta katika uchaguzi wa mkuu wa mwakani.

Gedion Moi, pia ni Mwenyekiti wa chama cha KANU, ambacho ndicho chama kilichotwaa madaraka kutoka mikononi mwa wakoloni na kuwa chama cha kwanza baada ya Kenya kupata uhuru.

Tangu mwaka 2013, Moi amekuwa akiwakilisha Jimbo la Baringo lililopo Magharibi ya Kati ya Kenya, ameonyesha nia ya kugombea urais, kuitawala Kenya kama alivyofanya baba yake chini ya chama hicho.

Mwaka 2013 na tena mwaka 2017, chama cha KANU kilimpigia debe rais aliyepo madarakani Uhuru Kenyatta, kuiongoza Kenya kwa mihula miwili madarakani.

Gideon Moi anajitosa kwenye kinyang'anyiro cha urais, jukwaa ambalo linashuhudia viongozi mbalimbali wa kisiasa waliokuwa ndani ya chama hicho miaka ya nyuma kama vile Naibu Rais wa Kenya William Ruto, Raila Odinga, Kalonzo Musyoka na Musalia Mudavadi.


Viongozi hao, wote wameonyesha nia ya kuwania kwa tiketi ya vyama tofauti kumrithi Rais Kenyatta, anayetarajiwa kustaafu mwaka 2022 baada ya kuwa madarakani kwa kipindi cha miaka 10.

Mark Bichache, mfuatiliaji wa siasa za Kenya anaeleza kuwa japo Moi hana nguvu kubwa za kisiasa, hafai kupuuzwa.

Kiongozi chama cha Orange Democratic Movement, Raila Odinga, aliyekuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, akizungumza katika hafla hiyo, alisema anaunga mkono kuwapo kwa uhuru wa vyama vya siasa, kudumisha demokrasia ya vyama vingi na anajivunia mwamko wa siasa za Kenya.

Kalonzo Musyoka, aliyekuwa Katibu Mtendaji wa chama hicho na sasa kiongozi wa Wiper Democratic, alieleza kuwa historia ya KANU ni chimbuko bora la historia ya Kenya.

Kiongozi wa Amani National Congress, Musalia Mudavadi, alisema vuguvugu la kisiasa, liitwalo One Kenya Alliance ambalo linamjumuisha Moi, limepata nguvu mpya kuelekea uchaguzi mkuu. **VOA**



Gideon Moi ambaye ameteuliwa na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya chama cha KANU, juzi, kugombea urais katika uchaguzi wa mwaka 2022. **PICHA: MAKTABA**

# Ethiopia yawatimua maofisa wa UN

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

MAOFISA saba wa Umoja wa Mataifa (UN), wamepewa muda wa saa 72 kuondoka Ethiopia. Serikali ya nchi hiyo imedai ni kutokana na watumishi hao kujiingiza katika mambo ya ndani ya Ethiopia.

Wakati huo huo, shinikizo linaongezeka dhidi ya serikali ya Ethiopia kuhusu jimbo la Tigray.

Serikali ya Ethiopia imechukua uamuzi wa kuwafukuza maofisa hao wa UN, huku Wizara ya Mambo ya Nje ya Ethiopia ikisema wafanyakazi saba wa mashirika ya misaada UN wanatakiwa kuondoka ikiwa ni pamoja na Naibu Mratibu wa Misaada nchini humo Grant Leaty na mwakilishi wa shirika la watoto la UNICEF, Adele Khodr.

Katibu Mkuu wa UN, Antonio alielezea hofu yake, baada ya Ethiopia kutangaza kuwatimua wakuu saba wa shirika hilo.

"Shughuli zote za kibinadamu za Umoja wa Mataifa zinaongozwa na kanuni za kimsingi za binadamu, kutopendelea, na kwa uhuru," alisema António Guterres,

"Nchini Ethiopia, Umoja wa Mataifa unatoa misaada ya kuokoa maisha ya watu- ikiwa ni pamoja na chakula, dawa, maji na vifaa vya usafi - kwa wale wenye uhitaji mkubwa."

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU** KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL). KWA MAWASILIANO ZAIDI **TUPIGIE:0677 111 333 AU 0758 112 332**

**NYUMBA/MASHAMBA**

**NYUMBA INAUZWA,** NYUMBA INAUZWA IPO MWANANYAMALA KWA KOPA. INA VYUMBA VITATU VYA KULALA, SEBULE, JIKO, CHOO NDANI NA NJE. INA UMEME, MAJI NA FENCE. KWA MAWASILIANO **PIGA: 0754409991.**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

## KUPOTEA KWA CHETI



**JULIUS ANCYLEM MAYAKA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1185-0132** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia DAR ES SALAAM BAPTIST SEKONDARI mwaka 2008. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **DAR/RB/474012/2021.**

116486702

## KUPOTEA KWA CHETI



**BAHATI M. MAKARANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0241-0009** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KOWAK GIRL'S SEKONDARI mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **DAR/CHU/RB/808513/2020.**

116487802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya MOROGORO**

**Kituo cha CHAMWINO Mkoa MOROGORO**

**Shauri la Madai Na. 25/2016**

**Jina la Mdai........................................NASMA AGUSTINO**

**Jina la Mdaiwa.....................................JESCAR DOMINIC**

**KATIKA SHAURI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa JESCAR DOMINIC**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba ( Eleza hapa habari za madai) YAH: KIWANJA KILICHOPO TUSHIKAMANE**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 15 mwezi 10 Mwaka 2021 saa 3:00 asubuhi/ mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 30 mwezi 09 mwaka 2021

HAKIMU

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO HANETI DODOMA

116488102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI.**

**Kituo cha DODOMA MJINI Mkoa DODOMA.**

**Usimamizi wa mirathi Na 200 /2021.**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MICHAEL YORAM.**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA DEOGRATIUS MICHAEL**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 05 mwezi 10 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 20 mwezi 09 mwaka 2021.

116488202

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**WUZHOU INVESTMENT COMPANY** LIMITED ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 350 BPW.** KWA YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **KAH/RB/496/2021.**

116488502

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ELIAS ALPHONCE MABULA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YAGARI AINA YA FUSO MITSUBISH YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 956 BJT.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI **KAH/RB/481/2021.**

116488402

## KUPOTEA KWA VYETI

Uongozi was shule ya sekondari **Cornelius Academy** and High School unatangaza kupotelewa na vyeti tarehe **13/04/2021** kutokana na wizi ulitokea shuleni hapo na kuripotiwa kituo cha polisi madale jalada **MDL/IR/927/2021** Kama ifuatavyo:- 1. Cornelius secondary school CSEE 218-2019 vyeti 94; ACSEE 2020 vyeti 11; 2. Andrew Faza memorial secondary school CSEE 2019 vyeti 23; 3. Dar-es-salaam Prime secondary school CSEE 2016, 2017 and 2018 vyeti 53;
Wasiliana na uongozi wa shule kupitia **0752517463 au 0786183747**

116487902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya MOROGORO**

**Kituo cha CHAMWINO**
**Mkoa MOROGORO**

**Shauri la Madai Na. 25/2016**

**Jina la Mdai........................................NASMA AGUSTINO**

**Jina la Mdaiwa.....................................JESCAR DOMINIC**

**KATIKA SHAURI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa JESCAR DOMINIC**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba ( Eleza hapa habari za madai) **YAH: KIWANJA KILICHOPO TUSHIKAMANE**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 15 mwezi 10 Mwaka 2021 saa 3:00 asubuhi/ mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 30 mwezi 09 mwaka 2021

116486502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IPYANA MSANIEGE MWAKILA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 171 BHB.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **MBEYA/KYE/RB/470208/2021.**

116487302

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**FATUMA ISSA SALUM** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina **MITSUBISHI CANTER** yenye namba za usajili **T 472 DFU.** Chassis no. **FE537B501985.** Engine No. **FE537B1985** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/472749/2021.**

116486602

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.
Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake amekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.
Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka Mke Wangu-13

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Baada ya kuridhika na kila kitu walichokiona, waliingia kwenye meseji. Baada ya kukutana na meseji nyingi zingine za kufurahisha, kuchekesha na kusikitisha, walikutana na zile ambazo walizihitaji.

Yalikuwa ni majibizano ya Sam na Farida.

"Mwaka wa kumi sasa unasema utanioa, lakini mpaka sasa naona kimya."

"Kwani wewe si mpenzi wangu? Kwani nimekuacha. Ukitaka si unakuja nyumbani, unakaa, unaondoka, kwani nikikuona nini kitakuwa kimepungua au kuzidi?"

"Sam unaniambia hivyo eee, yaani kwa sababu ukinihitaji unanipata, kwa hivyo umeniona kama mimi mwembe wako wa uani eee."

"Wewe si umeniuliza swali? Mimi nimekujibu. Ndoa huwa inakuja yenyewe siyo ya kulazimishana kama hivyo. Matokeo yake watu wanakaa wapenzi hata miaka 10, halafu wakioana mwaka huo huo wanapeana talaka Farida."

"Sasa nasema hivi. Mimi naondoka hapa Morogoro. Naenda kwa dada yangu Dar es Salaam. Ukinihitaji unanifuata. Kama hunihitaji basi, mimi nitakuwa nakaa huko huko, hapa Moro narudi tu kusalimia."

"Nini wewe?"

"Ndiyo hivyo hivyo nilivyoandika, nadhani umeelewa. Mimi nimechoka kukaa hivi hivi bila ndoa."

"Okay nenda huko Dar, lakini nakuhakikishia utarudi tu hapa Moro."

"Nitarudi kusalimia ndugu zangu, siyo kwako tena."

Hizo ni baadhi ya meseji ambazo Tom akiwa na mpenzi wake Tedi walizikuta kwenye simu iliyochukuliwa kwa Sam.


Yalikuwa ni malumbano ya meseji ya wapenzi wawili.

Picha ikamjia Tom kuwa mkewe Farida kabla ya kukutana Kigamboni maeneo ya Kibada akiishi kwa dada yake, alikuwa ametoka Morogoro kwa kugombana na bwana yake Sam.

Alikuwa ameondoka kutokana na kuchoka kuishi kukaa miaka mingi ya kuwa wapenzi bila kufunga ndoa.

Walizidi kuziangalia meseji ambazo zilionekana wakijizilana, ingawa kwa siku na nyakati mbalimbali.

"Nimeshapata mchumba mwezi wa nane naolewa."




**"Sasa mimi ningefanyaje? Ndugu zangu na kila mtu ameshajiandaa na harusi, mimi**

"Unasemaje wewe?"

"Nakwambia nimeshapata mchumba, wewe si unasuausa. Mwaka wa kumi, huna hata wazo."

"Farida, nakwambia hivi, wewe ni wangu tu, hata kama nikikaa miaka 20, lakini siku nikiamua kuwa nakuona ni siku moja tu, achana na hiyo habari, rudi Morogoro mara moja."

"Nasema sirudi ng'o, na tayari maandalizi ya harusi yanafanyika, naenda kuwa mke wa mtu tusitishane."

"Nakwambia hivi, nitahakikisha huolewi Farida."

"Utanifanya nini, unataka kuniua kabla ya ndoa?"

"Usinifundishe kazi, najua mimi nini itafanya."

Tom na Tedi waliendelea kuzipitia meseji zile za miezi mingi iliyopita. Kwa mbali, Tom alianza kupata picha.

Awali alikuwa anajiuliza ni kwa nini mkewe Farida alikuwa anafurahia ndoa. Na alikuwa anahimiza. Lakini ni kwa nini ghafla, wiki moja baada ya ndoa akatoroka bila kuaga.

Alikuwa akiwaza kama alikuwa hampendi kwa nini alikubali kuolewa? Na mbona ilionekana anampenda na hakukuwa na mgogoro wowote uliosababisha amtoroke?

Alianza kupata mwanga kuwa kulikuwa na shinikizo. Lilikuwa ni yeye kutoolewa. Aendelee kumsubiri Sam. Mwaka wowote akitaka atamuoa.

Tedi aliendelea kuzisaka meseji na kuzishusha. Alionekana kuwa mjuzi zaidi wa kuchezea simu za 'tachi' kuliko Tom.

Meseji zingine zikaonekana.

"Nini umefanya wewe. Umeolewa eee. Si nilikwambia acha hiyo habari?"

"Sasa mimi ningefanyaje? Ndugu zangu na kila mtu ameshajiandaa na harusi, mimi ningekataaje?"

"Sasa sikiliza nikwambie. Nazungumza hili kwa mara ya mwisho. Kwanza nilikuonya usiolewe. Ukakataa. Sitaki tuonane wabaya. Hili limekusamehe. Sasa narudia tena. Nakupa siku kumi tu, uwe umerejea Morogoro, safari hii hakuna msamaha utakaoupata."

"We unataka nifanye nini wakati nimeolewa?"

"Nani kakuoa wewe? Wewe ni wangu tu. Nataka umtoroke huko, uje huku."

"Huoni kama tunatengeneza matatizo makubwa"

"Hakuna tatizo hapo. Mimi si unanifahamu? Mimi ni mafia, kwa hiyo wewe njoo, mengine niachie mimi."

"Sam wewe lakini?"

"Hakuna cha lakini. Nakutumia picha za video sasa hivi. Hizi ndizo nitakazozivujisha kwenye mitandao ya kijamii kama usipotia mguu Moro siku kumi kuanzia leo."

Hapo ndipo Tom alipoelewa somo. Kumbe mkewe Farida alilazimika kumtoroka, baada ya bwana yake wa zamani Sam kutishia kusambaza picha chafu za video kwenye mitandao ya kijamii kama asiporudi kwake.

Alishusha pumzi kwa nguvu. Tedi alimtazama kwa huruma "Pole sana. Pole mpenzi." Alimtuliza.

Hakujibu kwa mdomo. Akatikisa kichwa. Kilichofuata ni video za picha ambazo Sam alitishia kuzisambaza.

Na zilionekana kweli kumtisha Farida, akamkimbia mumewe kabla ya hata piko aliyopaka haijakauka mwilini.

Nadhani aliona angekuwa mgeni wa nani kama zingevujishwa. Tena wakati huo yeye akiwa mke wa mtu. Na inawezekana ikaonekana kuwa zilikuwa zimepigwa baada ya harusi, au siku chache kabla ya harusi.

"Mimi nadhani mpaka hapa Tedi sina deni na wewe. Nashukuru sana sana tu. Umenisaidia sana. Sina uhakika kama ningekuwa peke yangu ningefanikisha kabisa. Au nisingefanikisha kwa muda mfupi kama huu.

Kilichonitoa Dar na kuja Moro ni kumsaka mke wangu. Nilimuona kwa njia ile ya kujibadilisha sura. Na nilitaka kujua ni kwa nini alinitoroka wiki moja baada ya harusi. Leo nimejua. Sina wa kumlaumu."

Maneno aliyoongea Tom kwa sauti ya huzuni, alianza kumliza Tedi. Aliangua kilio kana kwamba anaambiwa au anatuhumiwa yeye.

Ilibidi sasa Tom, aache simanzi aliyonayo na kuanza kumbembeleza. "Usilie Tedi. Haya yote ni ya dunia. Dunia ni tambala bovu. Lakini ipo siku yataisha na itabaki simulizi na kuandikwa tu kwenye vitabu na magazeti."

Walijikuta wakikumbatiana. Wakaachana na simu, makaratasi pamoja na picha. Waakaanza kubembelezana. Kila mmoja akimbembeleza mwenzake. Usingizi mororo ukawapitia.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# KABWAFA FC VS MAGAMAGA KUKATA UTEPE UMOJA CUP LEO

**Na Mwandishi Wetu**

MTIFUANO wa kuwania ubingwa wa Umoja Cup 2021 Wilaya ya Rorya mkoani Mara, unaanza kutimua vumbi leo kwa timu ya Kabwafa FC ya Shirati na Magamaga FC ya Sota kukata utepe wa michuano hiyo ambayo hufanyika kila mwaka wilayani humo.

Katika michuano hiyo ambayo itashirikisha timu 20 kutoka ndani ya Wilaya ya Rorya huku mechi zote zikipigwa Uwanja wa Maji Sota, mabingwa watetezi, Shirati Mji wataanza kutetea taji lao Oktoba 10, mwaka huu dhidi ya Bubombi FC.

Akizungumza na mwandishi wetu kuelekea michuano hiyo, Mwenyekiti wa mashindano hayo, Ochieng Melly, alisema timu hizo zimegawanywa katika makundi manne na timu mbili zitakazoongoza katika kila kundi zitatinga hatua ya mtoano. Alisema mbali ya wakazi wa Rorya kufurahia soka, lakini pia wapenzi wa mpira wa pete, watapata burudani ya kutosha watakaposhuhudia timu sita kutoka wilayani humo zikishindania taji hilo kwa upande wa wanawake.

Ochieng alisema mashindano hayo ambayo yamekuwa yakidhaminiwa na mdau maarufu wa soka wilayani humo, Peter Owino, kwa mwaka wa tisa sasa, yanatarajiwa kufikia kileleni mwanzoni mwa Desemba mwaka huu kwa mechi ya fainali kupigwa katika uwanja huo.

"Bingwa wa Umoja Cup atazawadiwa Sh. 350,000, mshindi wa pili Sh. 250,000 na mpira huku wa tatu akiibuka na Sh. 150,000, lakini pia kutakuwa na zawadi kwa mchezaji bora, mfungaji bora na timu yenye nidhamu, huku ikitolewa ngao ya heshima kwa mmoja wa watu waliochangia maendeleo ya soka Rorya kwa miaka mingi," alisema Ochieng.

Kwa upande wa Meneja wa Mashidano hayo, Daniel Obong'o, alisema mkakati wao ni kuifanya michuano hiyo kuwa mikubwa kwa siku zijazo.

Lakini mdhamini wa mashindano hayo, Owino, alisema matarajio yake kwa siku zijazo ni kuona michuano hiyo inashirikisha timu nyingi zaidi ikiwezekana kuwa na timu alikwa kutoka nje ya Wilaya ya Rorya ili kuongeza ushindani.

"Tunahitaji kupanua wigo kwa timu kuongezeka ili kuibua vipaji zaidi, lakini pia kudumisha undugu miongoni mwetu na kutoa ajira kwa vijana, kwani tangu kuanza kudhamini michuano hii miaka tisa sasa, vijana wengi wamenufaika kwa kupata timu za kubwa hadi za Ligi Kuu," alisema Owino.



Mchezaji wa timu ya Savana Boys, Mohamed Majili (kulia), akiusindikiza mpira wavuni huku akizongwa na mchezaji wa Ilala FC, katika mchezo wa ligi ya mchangani uliopigwa uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MRFA waomba umiliki uwanja wa Jamhuri

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

CHAMA cha Mpira Miguu Mkoa wa Morogoro, MRFA, kimewaomba wamiliki wa uwanja wa Jamhuri kuwakadhidhi eneo la kuchezea mpira (Pitch), ili kuondokana na changamoto ya kufungiwa kwa kutumika katika michezo ya ligi kuu Tanzania bara.

Ombi hilo lilitolewa jana na Katibu Mkuu wa MRFA, Emmanuel Kimbawala wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa, ambapo alibainisha miongoni mwa sababu za kufungiwa kwa uwanja huo.

Alitaja sababu hizo ni pamoja na wamiliki wa uwanja kukodisha uwanja huo kutumika katika matamasha mbalimbali ya kidini na burudani, ambao wamekua wakitumia eneo la katikati ya kiwanja bila kujali uharibifu wa nyasi katika eneo la kuchezea.

"Ni kweli kumekuwa na changamoto ya kufungiwa uwanja mara kwa mara, kwa sababu una matumizi mengi, wenzetu wamekuwa wakiukodisha kwa watu wa matamasha ya dini, mabonanza ya michezo na burudani ya muziki," alisema Kimbawala. Alisema kwa sasa marekebisho ya uwanja yamekamilika na muda wowote wanatarajia bodi ya ligi kuufungulia ili timu ya Mtibwa Sugar ianze kuutumia kama uwanja wa nyumbani, hivyo wamelazimika kuomba wamiliki kuwakabidhi ili waweze kuutunza.

"Sisi tumeshawaandikia Chama cha Mapinduzi (CCM) kuwaomba watukabidhi eneo la katikati ya uwanja la kucheza mpira, ili tuwe na udhibiti nalo ndio tutaweza kulitunza vizuri na kuondokana na kufungiwa mara kwa mara," alisema Kimbawala.

## Chirwa aanza na 'assist' mbili Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa klabu za Yanga na Azam FC, Mzambia Obrey Chirwa, ameanza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa staili ya aina yake, baada ya kutoa pasi mbli za magoli kwenye mechi ya kwanza akiichezea Namungo FC.

Jumatatu iliyopita kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi, Namungo iliichapa Geita Gold mabao 2-0, yaliyofungwa na Shiza Kichuya na Reliants Lusajo, pasi za mwisho za mabao yote ya mechi hiyo zikitoka kwa Chirwa.

Katika hali isiyo ya kawaida, kipa wa Mbeya City, Haroun Mandanda ameingia kwenye orodha ya wachezaji waliotoa pasi za mwisho, alipofanya hivyo kwenye mechi ambayo timu yake ilipata bao pekee dhidi ya mahasimu wao, Prisons kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya Jumanne iliyopita.

Sekunde chache kabla mechi kumalizika, kipa huyo alipiga mpira mrefu ambao ulimkuta Peter Mapunda aliyepiga kichwa mpira ukajaa ndani ya wavu, Mbeya City ikishinda bao 1-0.

Kabla ya mechi za jana, ni wachezaji saba waliotoa pasi za mwisho kwenye mechi za ufunguzi.

## Muumin sasa aamua kuangusha mojamoja

**Na Sabato Kasika**

MWIMBAJI nyota wa muziki wa dansi, Mwinjuma Muumin, amesema, wakati soko la muziki huo likiwa haliijasimama vizuri, bendi yake itaendelea kufyatua nyimbo mpya mmoja baada ya mwingine ili kuwa na nyimbo nyingi.

Akizungumza na gazeti hili jana, alisema, Special Band kwa sasa ina nyimbo mbili mpya tangu ikamilishe albamu Juni mwaka huu, alizozitaja kwa majina ya 'Hongera Mama Samia' na 'Salaam Maria'.

"Ninajua kuwa soko la muziki bado haliko vizuri, lakini hali hiyo haitukatishi tamaa, badala yake tutaendelea kufyatua wimbo mmoja baada ya mwingine ili kuhakikisha tunakuwa na nyimbo mpya za kutosha," amesema Muumin.

Amesema, bendi hiyo imekuwa ikifanya maonyesho ndani na nje ya Dar es Salaam ikitambulisha albamu mpya iitwayo 'Mkonga wa Tembo', lakini pia ikiandaa nyimbo mpya za albamu nyingine.

Muumin ametaja baadhi ya nyimbo zilizomo kwenye albamu hiyo ya kwanza yenye mchanganyiko wa vionjo kuwa ni 'Fenesi, Kwa Mparange Sihami na Vumbi la Congo'.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CAVANI ATAKIWA MADRID

REAL Madrid huenda wakafufua nia yao ya kumsaka mshambuliaji wa Manchester United na Uruguay, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 34 katika dirisha la uhamisho litakapofunguliwa Januari. (***El Nacional***)

### CHELSEA WAMJADILI RUDIGER

CHELSEA bado wanajadiliana na wakala wa beki wa Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28, kuhusu mkataba mpya. (***Fabrizio Romano via Twitter***)

### PHILLIPS KUSAINI LEEDS

KIUNGO wa kati wa England, Kalvin Phillips anakaribia kutia saini mkataba mpya na Leeds United kwa mujibu wa wakala wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 na tayari pande zote "ziko tayari" kufanikisha mpango huo. (***John Percy via Telegraph***)

### WERNER KURUDI UJERUMANI

MSHAMBULIAJI wa Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 25, ataangalia tena mustakabali wake katika klabu ya Chelsea kama atashindwa kuwa kwenye kikosi cha kwanza cha kocha, Thomas Tuchel - na huenda akarejea Ujerumani mwisho wa msimu huu. (***Telegraph***)

### KOEMAN ASUBIRISHWA

BARCELONA haitamfuta kazi kocha wake, Ronald Koeman raia wa Uholanzi kabla ya kukipiga na mabingwa wa LaLiga Atletico Madrid leo Jumamosi. (***Sport***)

### PELLEGRINI ATAKIWA WEST HAM

KLABU ya West Ham huenda ikapata nafasi ya pili ya kumsaini Luca Pellegrini mwenye umri wa miaka 22, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia akijidhatiti kupata nafasi ya kuchezea Juventus. (***Calciomercato***)

### NKETIAH KUSEPA

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Eddie Nketiah mwenye umri wa miaka 22, anataka kuondoka kwa washikabunduki hao wa London, huku klabu za Leeds, Aston Villa na Brentford zote zikifuatilia hali ya mchezaji huyo wa kimataifa wa England chini ya umri wa miaka 21. (***Ekrem Konur via Twitter***)

### KLOPP AMUWANIA DIABY

KOCHA wa Liverpool, Jugen Klopp anataka kumsajili winga wa Bayern Leverkusen na Ufaransa, Moussa Diaby mwenye umri wa miaka 22. (***Calciomercato***)

### PSG WALIMTAKA HERNDERSON

KLABU ya Paris St-Germain ilimtaka beki wa kati wa Liverpool na England, Jordan Henderson mwenye umri wa miaka 31, kabla ya kumsajili Lionel Messi mwenye umri wa miaka 34, kwa uhamisho wa bure kutoka Barcelona msimu huu. (***Goal***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SOUTHGATE: SANCHO HASTAHILI KUITWA KIKOSI CHA ENGLAND

Asema anahitaji kujiimarisha zaidi, bado hajaweza kuonesha kiwango chake kule Man United...

**LONDON,** England

KOCHA wa timu ya taifa ya England, Gareth Southgate, amekiri kwamba, Jadon Sancho ameitwa kwenye mechi za kimataifa ingawa hastahili nafasi hiyo kwa sababu ya kiwango chake.

Winga huyo mwenye umri wa miaka 21 amekuwa kwenye wakati mgumu tangu uhamisho wake wa fedha nyingi kutoka Borussia Dortmund na kutua Manchester United, akishindwa kufunga au kutoa asisti katika mechi nane za mashindano yote.

Ameshindwa kuonesha kiwango alichokuwa nacho kule Dortmund msimu uliopita, ambako alifunga mabao 16 na asisti 18 kwenye mechi 38 za mashindano yote Bundesliga, Ligi ya mabingwa na kombe la DFB-Pokal.

Sancho pia alianza katika mechi moja na mbili akitokea benchi katika kikosi cha England kilichotinga fainali ya Euro 2020 kabla ya kupoteza kwa Italia kwenye changamoto ya mikwaju ya penalti, akiwa mmoja waliokosa mikwaju hiyo.

**Southgate amemuita Sancho kwenye kikosi chake cha wachezaji 23 cha England kwa ajili ya michuano ya kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Andorra na Hungary.**

"Anastahili (kwenye kikosi cha England) kwa kiwango chake kwa wiki zilizopita? Pengine hapana," alisema Southgate.

"Lakini nafikiri tumewekeza kwa Jadon kwa ajili ya kipindi cha muda mrefu, tunaamini anaweza kuwa kwenye kiwango cha juu.


"Ningependa kuwa na muda na yeye na kuongea nae na kumsaidia kuendelea kuwa kwenye kiwango bora kule Manchester United na nataka yeye atambue kwamba tuna imani nae."

Southgate pia alibainisha kwamba, Sancho anahitaji muda zaidi wa kujiimarisha yeye mwenyewe baada ya kutoka Ujerumani na kuhamia kwenye Ligi Kuu ya England.

"Bundesliga ni tofauti kabisa, Dortmund ni klabu kubwa, lakini Manchester United ni moja ya klabu kubwa zaidi duniani," alisema Southgate.

MECHI KALI
HOME
AWAY
MANCHESTER UTD
1.56 | 4.07 | 5.88
EVERTON
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 537
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KANE ATAKA UMOJA SPURS



**LONDON, England**

HARRY Kane amesisitiza sasa ni wakati wa Tottenham kuwa nyuma ya Nuno Espirito Santo na kurudi kwenye kiwango chao Ligi Kuu ya England.

Straika huyo wa England alitokea benchi na kufunga mabao matatu 'hat-trick' na kuiongoza timu yake kupata ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Mura kwenye Ligi ya Europa Conference, Alhamisi.

Kane amekuwa mchezaji wa kwanza wa Spurs kufunga hat-trick akitokea benchi tangu Ronny Rosenthal alipofanya hivyo kwenye michuano ya FA mwaka 1995.

Mashabiki wa Spurs wanatumaini kiwango chake kitaendelea dhidi ya Aston Villa, Jumapili, kwani Kane ameshindwa kufunga katika mechi tano za mwanzo za Ligi England tangu msimu wa 2021-22.

Huku kukiwa na presha kubwa kwa kocha, Nuno baada ya kupoteza mechi tatu mfululizo za Ligi na kufungwa mabao tisa, Kane amesema mchezo dhidi ya Villa itakuwa sehemu ya kurudi kwako kwenye kiwango bora.

"Sisi kama wachezaji na benchi la ufundi tunahitaji kufanya kazi pamoja na kwa bidii," alisema Kane akiiambia BT Sport.

"Kiwango chetu cha hivi karibu hakijawa kizuri kwetu, lakini tunahitaji kujaribu katika mechi zinazokuja.

"Kila mshambuliaji anataka kufunga mabao. Pengine sikutarajia kuingia leo (juzi), lakini ni jambo zuri kwamba nilipata dakika.

"Wakati wote unapoona mpira unagonga nyavu za goli, unapata hisia nzuri sana. Matumaini yetu tutafanya hivyo wikiendi hii."

# Pele afurahia kutoka hospitalini



**SAO PAULO, Brazil**

GWIJI wa soka wa Brazil, Pele, amesema "nilikuwa napambania hewa" baada ya kuruhusiwa kutoka hospitalini, Alhamisi.

Mshindi huyo mara tatu wa kombe la Dunia alifanyiwa upasuaji wa kutoa uvimbwe kwenye ubongo na alikaa hospitalini kwa uangalizi maalumu pale katika hospitali ya Albert Einstein, mjini Sao Paulo.

Pele, ambaye amefikisha umri wa miaka 81, alikuwa na furaha kurudi uraiani na kuendelea kuwa kwenye uangalizi.

"Wakati mudа mgumu ukipita, sherehekea kila hatua kwenye safari ya maisha. Jikite zaidi kwenye furaha yako," aliandika Pele kwenye ukurasa wake wa Instagram.

"Ni kweli kwamba, siwezi tena kuruka, lakini siku chache zilizopita, nimekuwa nikiipambania hewa kuliko kawaida. Nina furaha kurudi tena nyumbani.

"Napenda kuishukuru timu yote kwenye hospitali ya Albert Einstein ambayo iliinisaidia kurudi kwenye hali yangu.

"Nawashukuru wote kutoka sehemu mbalimbali walionitakia kupona haraka."

Pele ndio mfungaji bora wa wakati wote wa kikosi cha Brazil, na alitikisa nyavu 77 katika mechi 92 alizoichezea nchi hiyo.

,737,060

# JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 02.10.21 | 17:00 | Derby vs Swansea | 2.52 | 3.22 | 2.72 |
| 2. 02.10.21 | 17:00 | Peterborough vs Bristol City | 2.57 | 3.21 | 2.67 |
| 3. 02.10.21 | 17:00 | Luton Town vs Huddersfield | 2.39 | 3.25 | 2.86 |
| 4. 02.10.21 | 17:00 | Hull City vs Middlesbrough | 2.86 | 3.25 | 2.39 |
| 5. 02.10.21 | 17:00 | Blackpool vs Blackburn | 2.86 | 3.16 | 2.45 |
| 6. 02.10.21 | 17:00 | Barnsley vs Millwall | 2.27 | 3.20 | 3.11 |
| 7. 02.10.21 | 18:00 | Montpellier vs Strasbourg | 2.40 | 3.47 | 2.78 |
| 8. 02.10.21 | 19:30 | Brighton vs Arsenal | 2.85 | 3.15 | 2.58 |
| 9. 02.10.21 | 22:00 | Atletico Madrid vs Barcelona | 2.14 | 3.32 | 3.47 |
| 10. 03.10.21 | 16:00 | Tottenham vs Aston Villa | 2.14 | 3.46 | 3.36 |
| 11. 03.10.21 | 16:00 | Crystal Palace vs Leicester | 3.21 | 3.46 | 2.20 |
| 12. 03.10.21 | 18:00 | Lille vs Marseille | 2.45 | 3.29 | 2.84 |
| 13. 03.10.21 | 18:30 | Liverpool vs Manchester City | 2.75 | 3.39 | 2.52 |

## MECHI ZA USHINDI


"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAMOSI - 02 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1741 | Manchester Utd vs Everton | 1.56 | 4.07 | 5.88 |
| 14:30 | 5788 | Coventry vs Fulham | 3.55 | 3.50 | 1.97 |
| 15:00 | 4717 | Osasuna vs Rayo Vallecano | 2.21 | 3.32 | 3.32 |
| 16:00 | 2514 | Salernitana vs Genoa | 2.96 | 3.16 | 2.50 |
| 16:00 | 4746 | Varbergs Bois vs Degerfors | 1.83 | 3.58 | 3.72 |
| 16:30 | 1581 | Hertha BSC vs SC Freiburg | 2.84 | 3.29 | 2.44 |
| 16:30 | 2190 | Dinamo Bucuresti vs UTA Arad | 4.91 | 3.48 | 1.70 |
| 16:30 | 2624 | Stuttgart vs Hoffenheim | 2.59 | 3.79 | 2.40 |
| 16:30 | 2755 | Cardiff Met Uni. vs Cefn Druids | 1.12 | 7.58 | 14.58 |
| 16:30 | 3170 | VfL Wolfsburg vs Monchengladbach | 2.16 | 3.43 | 3.23 |
| 16:30 | 4383 | Borussia Dortmund vs Augsburg | 1.21 | 6.75 | 10.92 |
| 17:00 | 1338 | KuPS Kuopio vs Ilves Tampere | 1.44 | 4.13 | 6.33 |
| 17:00 | 2845 | Cardiff vs Reading | 2.00 | 3.41 | 3.56 |
| 17:00 | 3328 | Blackpool vs Blackburn | 2.90 | 3.20 | 2.39 |
| 17:00 | 3538 | Hearts vs Motherwell | 1.58 | 3.85 | 5.52 |
| 17:00 | 3866 | QPR vs Preston | 2.06 | 3.37 | 3.42 |
| 17:00 | 4028 | Leeds vs Watford | 1.75 | 3.91 | 4.41 |
| 17:00 | 4051 | Luton Town vs Huddersfield | 2.09 | 3.41 | 3.31 |
| 17:00 | 4368 | Burnley vs Norwich City | 1.85 | 3.67 | 4.12 |
| 17:00 | 4384 | Hamilton vs Inverness | 3.46 | 3.36 | 2.01 |
| 17:00 | 4573 | Chelsea vs Southampton | 1.40 | 4.72 | 7.63 |
| 17:00 | 4636 | Hull City vs Middlesbrough | 3.01 | 3.06 | 2.40 |
| 17:00 | 5751 | Wolverhampton vs Newcastle | 1.67 | 3.97 | 4.92 |
| 17:15 | 2668 | Mallorca vs Levante | 2.14 | 3.33 | 3.48 |
| 18:00 | 1894 | Montpellier vs Strasbourg | 2.36 | 3.47 | 2.83 |
| 18:00 | 2470 | Admira Wacker vs SCR Altach | 1.89 | 3.58 | 3.49 |
| 18:00 | 2775 | Wolfsberger AC vs Austria Vienna | 2.17 | 3.39 | 2.95 |
| 18:00 | 4256 | Lokomotiva Zagreb vs Slaven Belupo | 1.95 | 3.39 | 3.49 |
| 18:30 | 2995 | Halmstads BK vs Ostersunds | 1.57 | 3.55 | 5.63 |
| 19:00 | 2922 | Grasshoppers vs St. Gallen | 2.29 | 3.34 | 2.95 |
| 19:00 | 3039 | Viking vs Sandefjord | 1.67 | 4.02 | 4.41 |
| 19:00 | 3418 | Besiktas vs Sivasspor | 1.86 | 3.56 | 3.91 |
| 19:00 | 3854 | CSKA Moscow vs FC Krasnodar | 2.32 | 3.40 | 2.86 |
| 19:00 | 4288 | Torino vs Juventus | 3.88 | 3.45 | 1.97 |
| 19:00 | 4788 | Sarpsborg vs Lillestrom | 2.46 | 3.35 | 2.71 |
| 19:30 | 1818 | Brighton vs Arsenal | 2.85 | 3.11 | 2.61 |
| 19:30 | 2809 | St Truiden vs Oostende | 2.12 | 3.64 | 3.05 |
| 19:30 | 3533 | Cadiz CF vs Valencia | 3.30 | 3.05 | 2.36 |
| 19:30 | 5573 | Spal vs Parma | 2.29 | 3.16 | 3.11 |
| 19:30 | 5773 | RB Leipzig vs VfL Bochum | 1.22 | 6.58 | 10.97 |
| 20:00 | 1539 | Porto vs Pacos Ferreira | 1.26 | 5.55 | 9.92 |
| 20:00 | 1859 | Viktoria Plzen vs Zlin | 1.37 | 5.01 | 7.61 |
| 20:05 | 5524 | Istra vs HNK Rijeka | 4.45 | 3.97 | 1.62 |
| 21:00 | 3589 | Heracles Almelo vs Willem II Tilburg | 1.92 | 3.55 | 3.65 |
| 21:30 | 2091 | FC Lugano vs Lausanne-Sport | 1.93 | 3.45 | 3.74 |
| 21:45 | 1640 | Sassuolo vs Inter | 4.14 | 4.14 | 1.75 |
| 22:00 | 3495 | Atletico Madrid vs Barcelona | 1.88 | 3.56 | 4.11 |
| 22:00 | 3852 | Nice vs Brest | 1.53 | 4.28 | 5.58 |
| 22:30 | 1156 | FC Arouca vs Sporting Lisbon | 7.28 | 4.23 | 1.43 |
| 22:30 | 3330 | Austin FC vs Real Salt Lake | 2.36 | 3.60 | 2.80 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# STURRIDGE APATA TIMU AUSTRALIA




**SYDNEY, Australia**

STRAIKA wa zamani wa Liverpool na England, Daniel Sturridge, amesaini katika Klabu ya Ligi Kuu ya Australia, A Legue, Perth Glory kwa ajili ya msimu wa 2021-22.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 amekuwa bila timu tangu alipoondoka katika Klabu ya Uturuki ya Trabzonspor, Machi, mwaka 2020.

"Ni nafasi nzuri kupata changamoto mpya,"alisema Sturridge.


Mmiliki wa Klabu ya Glory, Tony Sage alisema: "Daniel bila shaka ni moja ya usajili mkubwa katika historia ya Glory, lakini pia katika historia ya Ligi ya A-League."

Sturridge alitumia misimu sita na nusu akicheza Liverpool, akifunga mabao 67 katika mechi 160 kabla ya kuhamia kwa mkopo West Brom kwa kipindi cha pili cha msimu wa 2017-18.

Alihamia Uturuki mwaka 2019 akiwa mchezaji huru.

Mkataba wake wa miaka mitatu na Trabzonspor ulisitishwa Machi na nyota huyo wa zamani wa Manchester City na Chelsea alifungiwa miezi minne kutojihusisha na soka bada ya kuvunja sheria za michezo ya kubashiri.

"Wakati nafasi ikija, unahisi kama muda mwafaka kuuchukua, kuchukua kipaji changu sehemu nyingine ambako nirafurahia soka kwenye ligi ya ushindani na kujaribu kutafuta mafanikio zaidi," alisema Sturridge.




# Arteta: Kumkosa Xhaka ni pigo kubwa

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema kukosekana kwa Granit Xhaka kutakuwa "pigo kubwa" lakini amesisitiza washikabunduki hao watajitahidi kupambana bila kiungo huyo.

Xhaka atakuwa nje ya uwanja kwa miezi mitatu baada ya kuumia goti katika mchezo wa Jumapili wa ushindi dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja la London, Tottenham.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uswisi aliumia baada ya kugongana na Lucas Moura na nafasi yake ikachukuliwa na Albert Sambi Lokonga.

Xhaka atakosa mechi zote zilizobaki za Ligi Kuu kwa msimu wa 2021, ingawa klabu hiyo imethibitisha kwamba hatafanyiwa operesheni.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 ndio kwanza alikuwa amerudi uwanjani baada ya kufungiwa mechi tatu kwa sababu ya kuoneshwa kadi nyekundu kwenye mchezo dhidi ya Manchester City mwezi uliopita.

"Kwa uhakika ni pigo kubwa kumkosa Granit," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari.

"Yeye kukosekana kwake ni pigo kubwa sana kwetu. Tutakwenda kupambana bila yeye. Tutajaribu kuwa nae jirani wakati wote atakapokuwa akijiuguza."

# Michezo

Jumamosi Oktoba 2, 2021
Nipashe



Southgate: Sancho hastahili kuitwa kikosi cha England

UKURASA 21

# SIMBA SC YAANZA LIGI RASMI

## ●●●Ni baada ya sare, yaamka na kuifumua Dodoma huku...

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Kinyarwanda, Meddie Kagere, amekuwa mchezaji wa kwanza wa Simba kufunga bao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, alipopachika mpira ndani ya wavu dakika ya 70 na kuipa pointi tatu dhidi ya Dodoma Jiji kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma jana.

Ulikuwa mpira mrefu wa juu, ambao Chris Mugalu aliruka juu kuwazidi mabeki wa Dodoma na kumuwekea kwenye njia mfungaji ambaye bila ajizi akautumbukiza mpira wavuni.

Msimu huu Kagere anakuwa mchezaji wa kwanza kufunga bao kwa upande wa Simba, badala ya John Bocco ambaye alifanya hivyo msimu uliopita kwenye mechi ya kwanza ya Ligi Kuu, Septemba 6 dhidi ya Ihefu, Simba ikishinda mabao 2-1. Anamaliza ukame wa timu hiyo kucheza mechi tatu mfululizo bila kupata bao.

Kwanza ilikuwa ni Simba Day, ilipocheza dhidi ya TP Mazembe Septemba 20 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikifungwa bao 1-0, lakini ikichapwa idadi kama hiyo dhidi ya Yanga kwenye mechi ya Ngao ya Jamii Septemba 25, Jumanne iliyopita ililazimishwa suluhu bila kufungana dhidi ya biashara United kwenye mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara.

Kwa matokeo hayo, Simba inafikisha pointi nne, goli moja ikiwa haijafunga bao, huku Dodoma ikibaki na pointi zake tatu baada ya kushinda bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting, Jumanne iliyopita kwenye uwanja huo huo.

Ilikuwa ni kama vita, kwani wachezaji wa Dodoma waliamua kucheza mchezo wa kutumia nguvu zaidi kiasi cha kusababisha wachezaji watatu wa Simba kuumia.

Wachezaji hao ni Dadio Kanoute, Thadeo Lwanga na Kennedy Juma walioumizwa na kushindwa kuendelea na pambano.

Kutokana na hali hiyo, Simba ikalazimika kuwaingiza, John Bocco, Meddie Kagere na Duncan Nyoni kuchukua nafasi zao.

Rafu mbaya zaidi ilichezwa dakika ya 40 na Anuary Jabir aliporuka juu na kumpiga kiwiko, Kennedy. Beki huyo wa Simba hakuendelea na Anuary akazawadiwa kadi nyekundu.

Mchezaji Salmin Hoza naye alibahatika kumaliza dakika 90 bila kadi kutokana na rafu nyingi alizokuwa akicheza bila sababu yoyote ile.

Kocha Msaidizi wa Simba Selemani Matola amesema kuwa mchezo ulikuwa mgumu mithili ya vita na rafu zilikuwa zikichezwa kwa makusudi ili kuwatoa mchezoni, lakini wamefurahi kupata pointi tatu.

"Wenzetu hawakuja kucheza mpira, waligeuza kuwa mpira ni vita, lengo ni kututoa mchezoni, lakini leo muhimu kwetu ilikuwa ni kupata pointi tatu na ndivyo tulivyofanya," alisema.

Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Mbwana Makata alikiri kuwa kadi nyekundu aliyoipata mchezaji wake Anuary iliwafanya kuwa kwenye wakati mgumu na kusababisha kupoteza mechi.

Kwenye mechi nyingine iliyochezwa Uwanja wa Karume mjini Musoma, Biashara United baada ya kuivimbia Simba na kutoka suluhu Jumanne iliyopita, jana ilikiona cha moto ilipochapwa nyumbani bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting.

Lilikuwa ni bao la winga wa zamani wa Simba, Rashid Juma, baada ya pasi kutoka kwa Nathael Chilambo.



Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere, akishangilia bao pekee katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Dodoma FC iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga moto ule ule kwa Geita

**Na Saada Akida**

BAADA ya kushinda mchezo wa kwanza dhidi ya Kagera Sugar bao 1-0 Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, timu ya Yanga leo inatarajia kushuka dimbani kuikaribisha timu mpya kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, Geita Gold FC.

Mchezo huo utapigwa kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam majira ya saa 1:00 usiku.

Wao Geita Gold wanaoshiriki ligi hiyo kwa mara kwanza, walianza vibaya kwenye mchezo baada kukubali kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Namungo FC.

Timu hizo zinakutana kwa mara ya kwanza huku Yanga ambao ni wenyeji wa mchezo huo inayonolewa Kocha Mtunisia, Nesreddine Nabi na Geita Gold FC, iko chini ya Etienne Ndayiragije.

Makocha hao watakuwa na kazi ya ziada kila mmoja kuweka rekodi ya kushinda mchezo huo ambao Yanga inahitaji kujiweka sawa katika safari yao ya mbio za ubingwa.

Wakizungumza na gazeti hili makocha wa timu hizo, kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Geita Gold FC, Fred Felix Minziro, alisema vijana wote 23 wako salama na tayari kwa ajili ya kuwakabili Yanga.

Alisema wanaingia katika mchezo huo wakiiheshimu Yanga kutokana na ubora wa kikosi chao lakini haitawafanya kurudi nyuma na kuingia uwanjani kwa hofu.

"Yanga wana kikosi bora chenye wachezaji wazuri lakini hatuwezi kuwaogopa na tumewaandaa vijana wetu kama wakifuata maelekezo tunaenda kupata matokeo," alisema Minziro.

Kocha Mkuu, Nabi alisema sasa nguvu zinaelekea katika mchezo dhidi ya Geita Gold kuhakikisha wanakwenda kufanya vizuri ili kuibuka na ushindi.

Alisema wataendelea kukijenga kikosi na timu itazidi kuimarika sasa wakielekeza nguvu zao katika mchezo unaofuata kwa kupata matokeo chanya na kuibuka na ushindi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >